# MFUMO ANGAMI WA KIPEMBA NA ATHARI ZAKE KATIKA KUZUIA MAWASILIANO FANISI KWA WAGENI WA LAHAJA HIO

**AISHA AMEIR MOHAMMED**

**TASINIFU HII IMETOLEWA KWA MADHUMUNI YA KUTOSHELEZA BAADHI YA MASHARITI YA SHAHADA YA UZAMILI (M.A KISWAHILI-ISIMU) YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**2018**

## UTHIBITISHO

Aliyetia sahihi hapo chini anadhibitisha kuwa ameisoma kazi hii na anapendekeza kuwa Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania kukubali kupokea tasnifu hii: ***Mfumo Angami wa Kipemba na Athari zake katika Kuzuia Mawasiliano Fanisi kwa Wageni wa Lahaja hio***, katika kukamilisha baadhi ya matakwa ya shahada ya uzamili Kiswahili (Isimu) ya Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

**……………………………………………….………………….**

Dkt Mohamed Omary

**Msimamizi**

Tarehe ………………………………….

## HAKIMILIKI

Hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa namna yoyote sehemu yoyote ile ya tasinifu hii kwa njia yoyote kama vile, kielektroniki, kurudufu nakala, kurekodi au njia yoyote nyingine bila ya idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa niaba.

## TAMKO

Mimi, **Aisha Ameir Mohammed** natamka kuwa kazi hii ni yangu mwenyewe haijatolewa na haitotolewa kwa mahitaji ya kutunukiwa shahada ya uzamili au shahada nyingine ambayo ni sawa au karibu sawa na hii katika chuo kikuu chengine.

**…………………………………**

**Aisha Ameir Mohamed**

**Tarehe ……………………………..**

## TABARUKU

Natabaruku kazi hii kwa mama yangu mpenzi Zuhura Suleiman kwa upendo wake wa dhati aliokuwanao kwangu tangu utotoni hadi sasa. Aidha, naitabaruku kazi hii kwa baba yangu Ameir Mohammed. Pia kwa mume wangu kipenzi Mussa M. Abass na ndugu zangu Ameir, Mafunda na Raya kwa kuniunga mkono na kuniauni muda wote wa masomo.

Mwisho kwa watoto wangu wapenzi Zuhura na Salma.

# SHUKURANI

Kwa kuanzia ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uzima na kunipa uwezo wa kukamilisha utafiti huu. Kwa kiasi kikubwa ukamilishaji wa utafiti huu umetokana na msaada wa watu wengi. Nitakuwa mwizi wa fadhila endapo nitashindwa kuwashukuru watu ambao wamechangia ukamilishaji wa kazi hii.

Hatahivyo haitakuwa rahisi kuwataja wote kwa majina kwasababu ni wengi. Ninawashukuru wote nitakao wataja na wale nisiowataja waliochangia kufanikisha kazi hii kwa njia yoyote.

Ninatoa shukurani zangu kwa msimamizi wangu wa utafiti, Mw. Bakari Kombo kwa kukubali kuwa msimamizi wangu na kulisimamia pendekezo langu la utafiti na kunielekeza, kunishauri na kunikosoa katika kipindi chote cha utafiti huu pamoja na majukumu mengi aliyonayo. Ametumia busara na uvumilivu mkubwa hadi kufikia hatua ya kukamilika kazi hii. Vilevile ninawashukuru walimu wangu, wahadhiri wa Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania kwa kunifundisha kozi ya mbinu za utafiti ambayo iliniongoza katika uchambuzi wa data nilizozikusanya. Aidha, ninatoa shukurani kwa Dr Hadija Jilala na Dr Zelda Elisifa kwa kunifundisha kozi ya mofolojia na fonolojia ambazo zilinisaidia katika utafiti wangu. Pia sitowasahau Bi Amina Gogokwa msaada wao mkubwa walionipatia. Mwisho ninaishukuru familia yangu akiwemo Mume wangu bwana Mussa M. Abass pamoja na watoto kwa uvimilivu mkubwa waliouonesha wakati nikiwa katika shughuli za utafiti huu.

# IKISIRI

Utafiti huu unaohusu mfumo angami wa Kipemba na athari zake katika kuzuia mawasiliano fanisi kwa wageni wa lahaja hio, lengo lake kuu ni kuchambua mfumo angami katika lahaja ya Kipemba na jinsi mfumo huo unavyokwamisha mawasiliano kwa wageni wa lahaja ya Kipemba. Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya viangama ya Zwicky (1977) amechambua aina tatu za viangama ambavyo ni viangama awali, viangama kati na viangama tamati pia utafiti umebaini kuwa kuna tatizo la kimawasiliano kwa wageni wa lahaja ya Kipemba kutokana mfumo angami wa Kipemba. Utafiti umetumia mbinu mbalimbali katika ukusanyaji wa data zake. Utafiti umefanyika Mwambe, Chokocho, Kiuyu mbuyuni naKwale. Walengwa wa utafiti huu ni wazee, watu wa makamo na vijana. Kila shehia wamesailiwa watu 20wa umri na jinsia tafauti na kufanyiwa usaili watu 80. Utafiti huu umetumia mbinu za hojaji, usaili na ushuhudiaji. Utafiti umetumia data simulizi ambapo mtafiti amefanya usaili na kushuhudia kwa kusikiliza mazungumzo kutoka mikusanyiko ya watu mbalimbali. Data zilichambuliwa kimaelezo. Kwa upande wa matokeo ya utafiti, data zimeonesha kuwa kuna aina tatu za viangama katika mfumo angami wa Kipemba ambavyo ni viangami awali, viangami kati na viangami tamati aidha data zinaonesha kuwa kunajitokeza tatizo la kimawasiliano kwa wageni wa lahaja ya Kipemba kutokana na mfumo angami wa Kipemba. Kwa upande wa mapendekezo mtafiti amependekeza ufanyike utafiti wa mfumo angami wa lahaja nyengine. Pia anapendekeza kufanyike utafiti wa kutofautisha na kufananisha mifumo angami ya lahaja mbali mbali.

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| KP | Kipemba |
| KS | Kiswahili sanifu |
| Na | Nambari |
| Wke | Wanawake |
| Wme | Wanaume |
| TUKI | Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili |
| U | Umoja |
| W | Wingi |

## YALIYOMO

UTHIBITISHO ........................................................................................................ i

HAKIMILIKI ........................................................................................................ ii

TAMKO ... ........................................................................................................ iii

TABARUKU ........................................................................................................ iv

SHUKURANI ........................................................................................................ v

IKISIRI ..... ........................................................................................................ vi

ORODHA YA VIFUPISHO ........................................................................................................ vii

YALIYOMO ........................................................................................................ viii

ORODHA YA MAJEDWELI ........................................................................................................ xii

**SURA YA KWANZA: UTANGULIZI WA JUMLA ........................................................ 1**

1.1 Utangulizi wa Sura ........................................................................ 1

1.2 Usuli wa Tatizo ........................................................................ 1

1.3 Tatizo la Utafiti ........................................................................ 3

1.4 Malengo ya Utafiti ........................................................................ 5

1.4.1 Lengo Kuu ........................................................................ 5

1.4.2 Malengo Mahsusi ........................................................................ 5

1.4.3 Maswali ya Utafiti ........................................................................ 5

1.5 Umuhimu wa Utafiti ........................................................................ 6

1.6 Mipaka ya Utafiti ........................................................................ 6

1.7 Vikwazo vya Utafiti ........................................................................ 6

1.8 Utatuzi wa Vikwazo ........................................................................ 7

1.9 Mpangilio wa Utafiti ........................................................................ 7

**SURA YA PILI: MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA** ........ **8**

2.1 Utangulizi ........ 8

2.2 Fasili za Dhana ........ 8

2.2.1 Maana ya Mawasiliano ........ 8

2.2.2 Maana ya Lahaja ........ 9

2.2.3 Maana ya Kiangami ........ 9

2.2.4 Mfumo Angami ........ 10

2.3 Mapitio Kuhusu Ubainishaji wa Viangama ........ 10

2.4 Pengo la Utafiti ........ 14

2.5 Kiunzi cha Nadharia ........ 15

2.6 Hitimisho ........ 16

**SURA YA TAT: MBINU ZA UTAFITI** ........ **17**

3.1 Utangulizi ........ 17

3.2 Eneo la Utafiti ........ 17

3.3 Walengwa wa Utafiti na Usampulishaji ........ 18

3.4 Mbinu za Ukusanyaji Data ........ 19

3.4.1 Mbinu ya Uwandani ........ 19

3.4.2 Mbinu ya Maktabani ........ 19

3.5 Njia za Ukusanyaji Data ........ 20

3.5.1 Usaili ........ 20

3.5.2 Ushuhudiaji ........ 20

3.5.3 Hojaji ........ 21

3.6 Watoa Taarifa ........ 21
3.7 Uchambuzi wa Data ........ 22
3.8 Maadili ya Utafiti ........ 23
3.9 Hitimisho ........ 23

**SURA YA NNE: UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA ........ 24**
4.1 Utangulizi ........ 24
4.2 Mfumo Angami wa Kiswahili cha Kipemba ........ 24
4.2.1 Viangama Tamati Viwakilishi ........ 24
4.2.2 Viangama Tamati Vivumishi ........ 26
4.2.2.1 Viangama Tamati Vivumishi Vimilikishi ........ 27
4.2.2.2 Viangama Tamati Vivumishi vya Sifa ........ 33
4.2.2.3 Viangama Tamati Vivumishi Viulizi ........ 34
4.2.3 Viangama Tamati Vielezi ........ 35
4.2.3 Viangama Tamati Viunganishi ........ 41
4.2.4 Viangama Tamati Vitenzi ........ 42
4.3 Mfumo Angami Jinsi unavyokwamisha Mawasiliano Fanisi ........ 44
4.3.1 Kutofahamiana katika Mazungumzo ........ 46
4.3.2 Kuigawa Jamii na Kupoteza Muda ........ 47
4.3.3 Ufahamu Mbaya na Kujengeka Migogoro ........ 48
4.4 Ufaafu wa Nadharia Teule ........ 50
4.5 Baadhi ya Sentensi ambazo zinaonesha Ugumu wa Mawasiliano kwa Wageni wa Lahaja ya Kipemba ........ 53
4.6 Muhtasari ........ 55

**SURA YA TANO: MUHUTASARI WA UTAFITI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ..... 56**

5.1 Muhutasari wa Utafiti ..... 56

5.1.1 Muhutasari wa Kiujumla ..... 56

5.2 Muhutasari wa Matokeo ya Utafiti ..... 57

5.3 Hitimisho ..... 57

5.4 Mapendekezo ..... 57

**MAREJELEO ..... 59**

**VIAMBATANISHO ..... 63**

## ORODHA YA MAJEDWELI


Jedweai Na.3.1. Idadi ya Watoa Taarifa........................................................ 22

Jedwali Na:4.1 Viangama Vimilikikishi Nafsi ya Pili na ya Tatu Umoja ........ 30

Jedwali Na: 4.2 VivumishiVimilikisha vya Nafsi ya Pili ................................... 31

Jedwali Na: 4.3 Vivumishi Vimilikisha vya Nafsi ya Tatu ............................... 32

Jedwali Na: 4.4 Muhutasari wa Maumbo ya Viangama Mbalimbali ............... 44

Jedwali Na: 4.5 Pingamizi zinazojitokeza katika Mfumo Angami wa Kipemba ........................................................................................ 48

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI WA JUMLA

## 1.1 Utangulizi wa Sura

Sura hii inaeleza taarifa zinazohusiana na utafiti wa mada inayosema "Mfumo Angami wa Kipemba na Athari zake katika kuzuiya Mawasiliano Fanisi kwa Wageni wa Lahaja hiyo". Sura hii kwa ujumla imegusia vipengele muhimu ambavyo ni pamoja na utangulizi wa jumla wa mada ya utafiti, usuli wa tatizo la utafiti, tamko la utafiti, sura hii pia imeyaeleza malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti,mipaka ya utafiti, vikwazo vya utafiti pamoja na jinsi ya kuvitatua na kuvimalizia vikwazo hivyo. Vipengele vyengine vilivyobainishwa ni mpangilio wa utafiti nao pia utachambuliwa na kufafanuliwa katika eneo hili. Mwisho wa sura kutakuwa na hitimisho la sura.

## 1.2 Usuli wa Tatizo

Katika karne tuliyonayo tumeshuhudia kuwa Kiswahili ni moja miongoni mwa lugha tofauti duniani zinazotumika katika shughuli mbali mbali za kitaifa na kimataifa. Wanaisimu wanaofanya kazi kuchunguza lugha ya Kiswahili wamethibitisha kuwa Kiswahili ni lugha inayopokea mabadiliko makubwa kwa watumiaji wake. Hii ni kusema kuwa katika kipindi hiki tulichonacho lugha hii imeongeza idadi ya watumiaji, wakiwemo wazawa, pamoja na wageni wa lugha hii.

Mtafiti anakubaliana na wanaisimu wa Kiswahili kuwa Kiswahili ni lugha iliyobeba lahaja nyingi kadha wa kadha. Miongoni mwa lahaja hizo ni pamoja na Kipemba. Kwa mujibu wa Masamba (2004) Kipemba ni lahaja inayozungumzwa na wakaazi wanaoishi katika kisiwa cha Pemba.

Kwa kuwa Kipemba ni miongoni mwa lahaja za Kiswahili, basi watumiaji wa Kiswahili bila ya kujali kuwa ni wazawa au wageni wa Kiswahili hulazimika kukitumia Kipemba katika kukidhi haja yao ya mawasiliano. Kadri wageni wa lugha hii wanavyotumia lahaja ya Kipemba, kumegunduliwa kuibuka kwa malalamiko yanayoibuliwa na wageni wa lahaja ya Kipemba juu ya ugumu unaojitokeza katika kufahamu wanachozungumza wazawa wa lahaja hiyo.Kuna tafiti nyingi zilizofanywa katika lahaja ya Kipemba ambazo ziligundua kuwa viangama ni kipengele kimoja wapo kinachochangia katika kuzuia mawasiliano fanisi kwa wageni wa lahaja hiyo.

Katika kutathmini uzito wa jambo hili, kuna tafiti nyingi zilizofanywa juu ya mada ya viangami.Tafiti hizo hazikuwa tu katika lahaja ya Kipemba bali pia katika lahaja nyengine za Kiswahili.Ushahidi wa hayo ni pamoja na kazi ya Poleme (1967) ambae amechambua viangami viulizi na kiangama chenye maana ya vizuri katika methali za Kiswahili cha kale na kugundua kuwa kuna matumizi ya viangami tamati viulizi kama vile pi, ni na je katika Kiswahili cha kale. Makame (2015) alifanya uchambuzi wa viangama katika Kiswahili cha mazungumzo Unguja na amegundua viangama vimilikishi, viulizi, vivumishi, viunganishi na vielezi. Adi (2016) amechunguza viangama katika Kiswahili kinachoongelewa Tumbatu na amegundua kuwa katikaKiswahili Tumbatu hujitokeza viangama katika maumbo yafuatayo: Viangama tamati viwakilishi,vivumishi, vielezi, viunganishi na vitenzi. Said (2011) amefanya utafiti na amebainisha viangama katika lahaja ya Kipemba na kuonyesha viangama sahili. Mfano wa viangama sahili alivyogundua ni kama vile lo- inayojitokeza katika jikolo,ko- inayojitokeza katika nyumbaniko na yo- inayojitokeza katika sabuniyo.

Kwa kweli pamoja na kazi walizowasilisha watangulizi hawa juu ya mada ya viangama, lakini mtafiti kwa kiasi anachoelewa hajaona kazi yoyote inayohusu mfumo angami na jinsi unavyozuwia mawasiliano fanisi kwa wageni wa lahaja ya Kipemba. Kwa mantiki hii utafiti huu unadhamiria kuchunguza mfumo angami wa Kipemba na athari zake katika kuzuia mawasiliano fanisi kwa wageni wa lahaja hiyo.

## 1.3 Tatizo la Utafiti

Katika 1.2 mtafiti alikwisha kuainisha kuwa kuna tafiti mbali mbali duniani zilizojaribu kutafiti juu ya mada ya viangama katika lugha ya Kiswahili pamoja na lugha nyengine duniani. Kupitia maandiko mbali mbali mtafiti aliweza kugundua haya yafuatayo: Lambert (1957, 1958) Katika tafiti zake za lahaja za Kenya amechambua viangama tamati viwakilishi, vimilikishi na viulizi na akaweza kugundua kuwa kuna viangama nyuma viwakilishi na viangama nyuma vimilikishi katika lahaja hizo. Poleme (1967) amechambua viangami viulizi na kiangama chenye maana ya vizuri katika methali za Kiswahili cha kale na kugundua kuwa kuna matumizi ya viangama tamati viulizi kama pi, ni,na je katika Kiswahili cha kale. Pia wanazuoni kama Ashton (1977), Massamba na Wenzake (1990) na Massamba (2004) wamefasili na kutoa mifano ya viangama katika lahaja za Kiswahili. Said(2011) amefanya utafiti na amebainisha viangama katika lahaja ya Kipemba na kuonyesha viangama sahili. Mfano wa viangama alivyogundua ni lo kama inavyojitokeza katika -jikolo,ko- kama inavyojitokeza katika nyumbaniko na yo- kama inavyojitokeza katika neno sabuniyo.

Makame (2015) alifanya uchambuzi wa viangama katika Kiswahili cha mazungumzo Unguja na amegundua kuwa Kiswahili cha mazungumzo cha Unguja hujitokeza viangama katika maumbo yafuatayo: Viangama tamati viwakilishi, vimilikishi, viulizi, vivumishi, viunganishi na vielezi. Adi (2016) uchambuzi wa viangama tamati katika lahaja ya Kitumbatu na amebaini kuwa viangama tamati katika lahaja ya Kitumbatu vimejitokeza katika maumbo yafuatayo: Viangama tamati viwakilishi, vivumishi, vielezi, viunganishi na vitenzi. Kwa hivyo pamoja na jitihada za waandishi hao katika kuchambua mada ya viangami mtafiti amebaini kwamba hadi kufikia sasa watafiti wengi walijikita katika kuchunguza mfumo angami na viangama vinavyopatikana katika lugha zao tu. Katika kazi zote hizo hakuna utafiti ambao ulilenga kuainisha viangami vya lahaja ya Kipemba na kufafanua ni jinsi gani viangama vinavyokwamisha mawasiliano fanisi kwa wageni wa lugha.

Kama hilo halitoshi,vile vile kupitia maandiko mbali mbali mtafiti alishindwa kuona andiko maalumu ambalo lililenga katika kuchunguza mfumo angami katika lahaja ya Kipemba na athari zake katika kuzuia mawsiliano fanisi kwa wageni wa lahaja ya Kipemba.Tafiti hizo nyingi zilijikita katika kuangalia lugha ya Kiswahili kwa ujumla,pamoja na lugha nyengine zisizo kuwa Kiswahili na chache katika lahaja ya Kipemba lakini zote hizo hazikuangalia athari hizo za viangama katika lahaja ya Kipemba jinsi zinavyozuia mawasiiliano fanisi kwa wageni wa lahaja ya Kipemba.Kama hivyo ndivyo,basi utafiti huu ulilazimika kufanyika ili kusaidia kuweka bayana jinsi mfumo angami wa Kipemba unavyozuia mawasiliano fanisi kwa wageni wa lahaja hiyo.Utafiti huu kwa maana hio umekuwa ni utafiti wa

kwanza ambao unalenga katika kuchunguza mfumo angami wa Kipemba na athari zake katika kuzuia mawsailiano fanisi kwa wageni wa lahaja hiyo.

Kwa hali hii mtafiti amehisi ipo haja ya kuziba pengo hili, ndipo kwa dhati yake akaamua kuchunguza mfumo angami wa Kipemba na athari zake katika kuzuiamawasiliano fanisi kwa wageni wa lahaja ya Kipemba kwa lengo la kupunguza mwanya uliuoachwa na watangulizi wake.

## 1.4 Malengo ya Utafiti

### 1.4.1 Lengo Kuu

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza mfumo angami wa lahaja ya Kipemba na athari zake katika kuzuia mawasiliano fanisi kwa wageni wa lahaja ya Kipemba.

### 1.4.2 Malengo Mahsusi

i. Kubainisha mfumo angami wa lahaja ya Kipemba.

ii. Kuonesha mfumo angami jinsi unavyokwamisha mawasiliano fanisi kwa wageni wa lahaja ya Kipemba.

### 1.4.3 Maswali ya Utafiti

i. Ni upi mfumo angami unaojitokeza katika lahaja ya Kipemba?

ii. Ni vipi mfumo angami wa Kipemba unakwamisha mawasiliano fanisi kwa wageni wa lahaja ya hiyo?

## 1.5 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu utakuwa na umuhimu mkubwa sana kwa wanaisimu wengine watakaoamua kufanya utafiti utakaohusiana na viangami. Umuhimu huo utajitokeza katika vipengele vifuatavyo:

Utatumika kama kumbukumbu za kimaktaba zitakazowasaidia wasomi na wadau wengine wa elimu kupata marejeleo ya kiisimu hasa kwenye mada ya viangama. Utawasaidia walimu na wanafunzi kupata marejeleo yanayosaidia katika kazi ya kujifunza na kufundisha.

## 1.6 Mipaka ya Utafiti

Viangami vinaweza kujitokeza katika lugha tofauti ulimwenguni. Utafiti huu utashughulikia

viangami vinavyojitokeza katika Kiswahili cha Kipemba na jinsi unavyozuia mawasiliano fanisi kwa wageni wa lahaja hii.

Utafiti hautojishughulisha na viangami vinavyojitokeza katika lahaja nyengine za Kiswahili zisizokuwa Kipemba.

## 1.7 Vikwazo vya Utafiti

Kwanza ni ugumu wa kupatikana marejeleo kama vile tasnifu na vitabu mbalimbali vinavyohusiana na mada hii. Kikwazo hiki kinatokana na kutokuwepo kwa marejeleo hayo katika kisiwa cha Pemba ambako ndio eneo analoishi Pili ni tatizo la kifedha, hili ni tatizo kubwa kwani kazi hii itamlazimu mtafiti asafiri kwenda nje ya eneo la Pemba kwa mfano Dar-es-salaam na Zanzibar hali inayohitaji fedha nyingi mtafiti

## 1.8 Utatuzi wa Vikwazo

Katika kutatua kikwazo la kwanza mtafiti alitumia mitandao kwa ajili ya kupata marejeleo mbali mbali zikiwemo tasnifu, makala pamoja na vitabu mbali mbali. Mtafiti pia alitembelea katika maktaba kuu ya serikali iliopo Pemba pamoja na maktaba nyingine kama ile ya chuo cha ualimu cha Benjamin Mkapa ambacho kimepanda hadhi na kuwa sehemu ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA).

Katika kutatua kikwazo chas pili mtafiti alikusanya fedha kutoka mfukoni mwake pamoja na kuomba misaada kutoka kwa wahisani mbali mbali wakiwemo ndugu, jamaa na marafiki kuweza kukamilisha utafiti huu.

## 1.9 Mpangilio wa Utafiti

Kazi hii ya utafiti itawasilishwa katika sura tatu. Sura ya kwanza itatoa taarifa za jumla kuhusu utafiti huu. Inaelezea tatizo linalohitaji kufanyiwa utafiti, malengo ya utafiti pamoja na kuelezea umuhimu wa utafiti. Ndani ya sura hii ya kwanza kutakua na mambo mengi yanayohusiana na taarifa za awali za utafiti ikiwemo usuli wa tatizo. Sura ya pili inaelezea juu ya mapitio ya kazi mbali mbali zilizofanywa na zenye uhusiano na utafiti huu na sura ya tatu inamalizia kwa kuelezea mbinu za utafiti zitakazotumika katika kukusanya data pamoja na kuelezea jinsi ya kuzichambua data zitakazopatikana kutoka katika eneo la utafiti.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA

## 2.1 Utangulizi

Sura hii imeelezea mapitio mbali mbali ya maandishi ambayo yalihusiana na mada ya utafiti. Sura hii pia ilijadili kiunzi cha nadharia kilichoongoza uchambuzi wa data za utafiti huu. Mapitio ya kazi tangulizi zitlizoangaziwa yalimuwezesha mtafiti kutambua fasili ya viangama, kuainisha viangama na kubaini jinsi viangama vilivyowahi kuangaziwa katika kazi hizo. Mapitio ya kazi tangulizi pia yalimuwezesha mtafiti kujua utafiti uliofanywa katika eneo hili. Kazi tangulizi zlimuwezesha mtafiti kuepukana na kurejea kazi ambazo zimeshawahikujadiliwa na watafiti tangulizi. Kuzipitia kazi hizo kulitoa mwanga uliomuwezesha mtafiti wa kazi hii kubainisha viangama katika maneno mbali mbali ndani ya lahaja ya Kipemba pamoja na athari za viangama kwa wageni wa lahaja ya Kipemba na jinsi viangama vinavyozuia mawasiliano fanisi kwa wageni wa lahaja ya Kipemba. Sura hii pia itahusika na ubainishaji wa kipengele cha pengo la utafiti.

## 2.2 Fasili za Dhana

### 2.2.1 Maana ya Mawasiliano

Mawasiliano ni mchakato wa kupeleka au kupokea taarifa kutoka kwa mmoja kwenda kwa mwengine kwa kutumia nyenzo maalum. Mawasilano yanawewza kuwa ya mdomo kwa mdomo au kutumia vifaa maalum kama simu, redio, barua na vyenginevyo (Poleme, 1967). Kwa mujibu wa Gutfrik (1948). Mfumo ni mjumuisho wa sehemu au vitu tofauti vyenye uhusiano ambavyo hufanya kazi kwa pamoja ili kujenga sehemu moja ya kitu.

### 2.2.2 Maana ya Lahaja

Lahaja ni aina ya lugha inayozungumzwa na kundi la watu na ndani yake kuna msamiati, sarufi na matamshi (Webster,2014). Ingrams. (1924), kwa upande wake anasema kwamba lahaja ni vilugha vidogo vidogo vya lugha moja ambavyo hubainika katika jamii.

### 2.2.3 Maana ya Kiangami

Anderson (2005) amefafanua kiangami kuwa ni kipashio ambacho hakifungamani na sentensi kwa njia ya kawaida ya mfungamano wa maneno kama ambavyo viambishi hufungamana. Anderson (keshatajwa) amewagawanya wataalamu walioelezea viangama katika makundi mawili ambayo ni kundi la wanafonolojia na wanasintaksia. Wanafonolojia wanaona kuwa viangami ni maneno madogo ambayo hayana mkazo wake pekee mpaka yaegemee katika maneno yanayopakana nayo. Kwa mfano mtotowe, kiticho, chakulacho na mengineyo.Wanasintaksia wanaona kuwa kiangama ni kipashio ambacho mara nyingi huhusiana na viwakilishi vya nomino na vipashio vyengine vyenye sifa kama hiyo. Kazi ya Anderson (keshatajwa) itamsaidia mtafiti kueleza fasili ya kiangama na kubainisha baadhi ya maneno ambayo hubeba viangami.

Masamba (2004) amefasili kiangama kuwa ni umbo ambalo linafanana na neno lakini si neno kwa maana kwamba haliwezi kusimama peke yake likaleta maana. Umbo hilo hutegemea ama neno lililo nyuma yake au mbele yake. Pamoja na kwamba linafanana na kiambishi lakini uamilifu wake ni zaidi ya kiambishi. Kwa mfano viambishi an nathe katika Kiengereza havina maana vikisimama peke yake; au viambishi –ko katika neno nyumbaniko, -wo katika neno mtotowo katika

Kiswahili navyo havina maana na haviwezi kusimama peke yake. Kazi ya Massamba (keshatajwa) ili msaidia mtafiti kuweza kuelewa maana ya kiangama,kubainisha viangama halikadhalika kueleza mifano ya maneno yanayoweza kubeba viangama.

### 2.2.4 Mfumo Angami

Fromkin na Wenziwe (2000) wamefasili uangamaji kuwa ni uegemezaji wa mofimu kwa neno jingine au mofimu nyingine kifonolojia au kimatamshi. Kwa mfano, the cow = th'cow, pia wamefafanua kuwa katika Kiengereza kuna uangamaji unaotokana na ukataji wa neno. Kwa mfano 's inayotokana na (is) ambapo inaandikwa it's drinking, or 've inayotokana na (have) inayoandikwa we've. Kazi ya Fromkin na wenziwe (wameshatajwa) ilimsaidia mtafiti kuelewa maana ya viangama na vigezo vya kuvibainisha viangama.

## 2.3 Mapitio Kuhusu Ubainishaji wa Viangama

Mapitio yanayohusu ubainishaji wa viangama katika lugha mbalimbali kama vile Kihispania, Kikatalani, Kiingereza na lahaja za Kiswahili kama vile Kivumba, Kingare, Chijomvu, Kipemba na Chichifundi. Lopez (2008) amechunguza kiangama katika kihispania na kuonesha nafasi ya viwakilishi kwenye lugha ya Kihispania ambapo amebaini kuwa Kihispania kinyume na lugha za Kirumi, kinaruhusu kiangama kuungwa na vitenzi visio ukomo na vitenzi vilivoambikwa na vinaweza kuhama nafasi yake. Kwa mfano:

**Data 1**

Lo estoy comiendo = ninakula

Quiero Comerlo = natakakula

Kazi ya Lope'z (keshatajwa) itamsaidia mtafiti kubainisha viangama mbali mbali vinavyoungwa na vitenzi visivyo ukomo na vitenzi vilivyoambikwa katika lahaja ya Kipemba. Wheeler na wenziwe (1999 na Anderson (2005) wametafiti viangama katika lugha ya Kikatalani ambayo pamoja na kuwa na viangama vingine, lakini wataalamu hawa walivutiwa zaidi na sifa ya viwakilishi kukaa kabla ya kitenzi katika kishazi wakati ambapo hakikutumia viangama hakiwezi kuwa na muundo huo. Kazi ya Wheeler na wenziwe (wameshatajwa) ilmsaidia mtafiti kubaini aina mbali mbali za viangama na maneno ambayo hubeba viangama katika lahaja ya kipemba.

Lambert (1957) alipokuwa akichambua lahaja za Kivumba, Kingare, Chijomvu na Chichifundi amebainisha viangama nyuma viwakilishi na viangama nyuma vimilikishi katika lahaja hizo. Kazi ya Lambert (keshatajwa) itamsaidia mtafiti kubainisha viangama kwenye viwakilishi katika lahaja ya kipemba. Polome (1967) na Ashton (1977) wakichambua lahaja kama Lambert (1958) wamebainisha viangama tamati viulizi ambavyo ni pi, ni na je. Kazi ya Polome na Ashton itamsaidia mtafiti kuchambua viangama tamati pi, ni na je katika lahaja ya Kipemba.

Fronkin na wenziwe (2000) wameeleza kuwa katika lugha nyingi kuna viangama vinavyoungwa na virai vingine au sentesi nyingine. Katika lugha ya San Lucas Quiavini Zapotec, kiangama – zhyi chenye maana ya lazima huungwa na neno la mwanzo katika kirai. Kwa mfano:

**Data 2**

Banguual-zhyi naa Gyeeihlly

Old - must be Michael

Gyeeihlly –zhyi naa banguual

Michael lazima ni mzee

Naa -zhyi Gyeeihlly banguual

Be – must Michael old

Katika sentesi (a) kiangama kimeungwa na neno banguual (mzee) ambalo ni nomino, katika sentesi (b) kiangama kimeungwa na neno Gyeeihlly (Machael) ambalo ni jina la pekee na katika sentensi (c) kiangama kimeungwa na neno naa (ni) ambalo ni kitenzi kishirikishi kuwa. Kazi ya Fromkin na wenziwe ilimsaidia mtafiti kubainisha viangama tofauti pamoja na kubainisha maneno yanayobeba viangama katika lahaja ya Kipemba halikadhalika na kufafanua athari zake katika kuzuia mawsiliano fanisi kwa wageni wa lahaja ya Kipemba.

Katamba na Stonham (2006) wanaeleza kuwa kuna viangama vinavyoegemea kategoria mahususi, lakini pia kuna viangama vinavyoegemea kategoria tofauti. Kwa mfano katika Kiengereza kiangama'‘s kinachotokana na msinyao wa kitezi kishirikishi ‘is’ au ‘has’ kwa kawaida huegemea nomino. Kwa mfano:

**Data 3**

Asha’s playing = Asha is playing

I’ve books = I have books

Pia msinyao wa kitenzi kishirikishi unaweza kuegemea viunganishi, vitenzi, vivumishi na vielezi katika Kiengereza. Kazi ya Katamba na Stonham ilimsaidia mtafiti kubainisha viangama pamoja na maneno ambayo hubeba viangama katika lahaja ya Kipemba. Lambert (1957) ameonesha viangama vinavyoegemea vitenzi, nomino, vielezi na viunganishi. Kwa mfano:

**Data 4**

Chiricho = Kiti chako

Vecheo = peke yako

Nami = Na mimi

Kazi ya Lambert ilimsaidia mtafiti kubainisha viangama vinavyoegemea nomino, vitenzi, vielezi, viunganishi, viwakilishi na vihisishi katika lahaja ya Kipemba.

Masebo (2007) anaonesha viangama vinavyoegemea vitenzi na nomino katika Chindali. Kwa mfano:

**Data 5**

Mikokwejo = Mti mwembamba

Mulishaki = Mwanamme gani

Akulimakwo = Analima kule

Kazi ya Masebo ilimsaidia mtafiti kubainisha viangama vinavyoegemea nomino na vitenzi katika lahaja ya Kipemba. Pia mtafiti aliweza kufafanua athari za viangama katika kuzuia mawasiliano fanisi kwa wageni wa lahaja ya Kipemba.

Said (2011) aliangalia viangama tamati katika lahaja ya Kipemba na kuonesha viangama sahili.Kwamfano lo kama inavyojitokeza katika neno - jikolo, cho- kama inavyojitokeza katika neno chakulacho na po- kama inavyojitokeza katika neno mahalipo.

Makame (2015) katika utafiti wake unaohusu viangama katika Kiswahili cha mazungumzo cha Ungujana amegundua kuwa katikaKiswahili cha mazungumzo cha Unguja hujitokeza viangamakatika maumbo yaViangama tamati viwakilishi, vimilikishi, viulizi, vivumishi, viunganishi na vielezi.

Adi (2016) ambaye alichunguza viangama tamati katika lahaja ya Kitumbatu amebaini kuwa  viangama tamati katika lahaja ya Kitumbatu vimejitokeza katika maumbo yafuatayo: Viangama tamati viwakilishi, vivumishi, vielezi, viunganishi na vitenzi.

## 2.4 Pengo la Utafiti

Licha ya kuwepo wanaisimu ambao walichunguza viangama katika lahaja ya Kipemba lakini walionekana kuchunguza baadhi tu ya maeneo na sio mfumo angami na jinsi unavyokwamisha mawasiliano kwa wageni wa lahaja ya Kipemba na ndio sababu mtafiti akaamua kufanya uchunguzi kuhusiana na mfumo angami wa Kipemba na athari zake katika kuzuia mawasiliano fanisi kwa wageni wa lahaja hiyo.Kuhusu lahaja ya Kipemba watafiti hao wameonekana kuchunguza lahaja hii katika baadhi tu ya maeneo na sio kiujumla, pia hawakuchunguza athari zake katika kuzuia mawasiliano fanisi kwa wageni wa lahaja hiyo.

Kwa sababu hiyo mtafiti wa kazi hii anakusudia kupunguza mwanya ulioachwa na watafiti wengine kwani lengo lake ni kuchunguza Mfumo angami katika lahaja ya kipemba na athari zake katika kuzuia mawasiliano fanisi kwa wageni wa lahaja ya kipemba.Hii ni kwasababu eneo hili bado halijawahi kufanyiwa uchunguzi na watafiti tangulizi hata kwa wale wachache waliochunguza viangama katika lahaja ya Kipemba hawajawahikufafanua athari hizo.

## 2.5 Kiunzi cha Nadharia

Mushengezi (2003) yeye amesema kuwa nadharia ni maarifa yaliyopangwa ili kueleza dhamira fulani au wazo fulani."Nadhria ni mawazo, maelezo au muongozo uliopangwa ili kusaidia kueleza, kutatua au kutekeleza jambo fulani"(Kamusi la Kiswahili Sanifu 2004:200). Utafiti huu ulitumia nadharia ya kiangama ya Zwicky (1977). Zwicky ni kati ya wanaisimu wa awali walioandaa kazi zao kwa ufafanuzi juu ya sifa za kiangama. Mwanaisimu huyu alifafanua zaidi juu ya sifa za neno na kiambishi na kubainisha kuwa kuna maumbo ambayo ni tata yamechanganya sifa za maneno na viambishi na kuyaita viangama. Alieleza kuwa kuna sulubu tatu za viangama: viangama sahili, viangama maalumu na maneno funge.

Nadharia ya Zwicky (1977) imeshatambulika na wanaisimu wengi kwa vile imetumiwa na wataalamu tofauti kama Spencer (1991), Anderson (2005), Katamba na Stonham (2006) wanaeleza kuwa mwanaisimu huyu alieleza kwamba, lugha zote zinatofautiana katika baadhi ya vipashio vya lugha hizo lakini kuna mofimu ambazo zina ugumu katika kuchambua kwake ambazo ndio viangama. Watalamu hawa wameeleza kuwa kuna viangama sahili na viangama maalumu. Wameeleza pia kuwa viangama vinavyoungwa mwanzoni mwa neno ni viangama awali na vile

vinavyoungwa mwishoni ni viangama tamati.Said (2011), Makame (2015) na Adi (2016). Anderson (2005) ameeleza vipengele vya kinadharia vya viangama, na kubainisha aina za viangama kama zilivyoelezwa na Zwicky (1977) yaani viangama sahili, viangama maalumu na maneno funge.

Utafiti huu ulitumia  Nadhara ya viangama ya Zwicky (1977) iliyofafanuliwa na Katamba na Stonham (2006). Nadharia hii ilimuwezesha mtafiti kubainisha mfumo viangami katika lahaja ya Kipemba na kuelezea jinsi  mfumo viangami unavyozuia mawasiliano fanisi kwa wageni wa lahaja ya Kipemba. Katika kubainisha maneno ambayo hubeba  viangama alitutumia uchambuzi wa maneno kama ambavyo umefafanuliwa na Kihore (2009) kwa sababu Katamba na Stonham wanaeleza viangama katika lugha za Ulaya. Hii ni kwasababu maneno ya Kiswahili yanatofautiana na maneno ya lugha za Ulaya.

## 2.6 Hitimisho

Sura hii imehusika na mapitio ya maandiko na machapisho mbali mbali yanayohusiana na mada ya utafiti huu pamoja na nadharia ilioongoza utafiti. Katika utafiti juu ya mada husika, maandiko na machapisho mbali mbali yanayohusiana namfumo angami wa Kipemba yamefafanuliwa kwa kirefu kwa hivyo basi kazi tangulizi zilizofafanuliwa kwa kina ni juu ya  mfumo angami wa Kipemba na athari zake katika kuzuia mawasiliano fanisi kwa wageni wa lahaja hiyo.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Katika sura hii mtafiti alibainisha hatua, njia na mbinu mbalimbali zilizotumika katika kukusanya, kuchambua na kuwasilisha data za utafiti ili kuchunguza mfumo angami wa lahaja ya Kipemba na jinsi unavyozuia mawasiliano kwa wageni wa lahaja hiyo. Vipengele vilivyofafanuliwa hapa ni eneo la utafiti, walengwa wa utafiti na usampulishaji.Mambo mengine yaliyojadiliwa hapa ni mbinu za ukusanyaji data, vyanzo vya data, mbinu za uchambuzi wa data, uwasilishaji wa data na maadili ya utafiti.

## 3.2 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulifanyika katika shehia nne za Pemba.shehia hizo ni ni Kiuyu Mbuyuni na Kwale kwa upande wa kaskazini na shehia ya Mwambe na Chokocho kwa upande wa kusini Pemba.

Kisiwa cha Pemba kipo katika bahari ya hindi,upande wa magharibi. Kisiwa hicho kimepakana na mwambao wa Tanzania bara kama vile Tanga, kaskazini magharibi Pemba imepakana na Mombasa,upande wa kusini kimepakana na kisiwa cha Unguja ambacho kipo takribani kilomita 40,upande wa kaskazini mashriki.Kisiwa cha Pemba kimepakana na bahari yenye mkondo mkali kuanzia kusini hadi kaskazini mashariki.Hali ya hewa ya kisiwa cha Pemba si yenye kutabirika kwani inapata mvua nyingisana hasahasa katika miezi ya Machi,Aprili na Mei na joto kali wakati wa Novemba  Disemba na Januari.Shughuli za kiuchumi za watu wa kisiwa hiki cha Pemba ni kilimo,uvuvi, biashara na ufugaji. Kisiwa cha Pemba kina jumla ya mikoa

miwili yaani kaskazini Pemba  na kusini Pemba. Mkoa wa Kaskazini Pemba umeundwa na wilaya mbili ambazo ni wilaya ya Wete na wilaya ya Micheweni. Mkoa wa Kusini Pemba umeundwa na wilaya mbili, nazo ni wilaya ya Mkoani na wilaya ya Chake Chake. Utafiti huu ulifanyika katika mikoa yote miwili ya Pemba. Utafiti huu ul[fanyika katika maeneo haya kwasababu wazungumzaji wake wanaonekana kuingiza viangama kwa wingi zaidi katika mazungumzo yao.

### 3.3 Walengwa wa Utafiti na Usampulishaji

Kwa mujibu wa Cooper (1989) na Vans (1990), walengwa wa utafiti ni wanachama wote, mtu mmoja, kikundi au elementi ambazo mtafiti amekusudia kuzihusisha katika utafiti wake. Walengwa waliotumiwa katika kazi hii ni watu wa rika tofauti, wakiwemo wazee,watu wa makamo na vijana.Utafiti huu ulitumia usampulishaji nasibu pangilifu na usampulishaji eneo. Watafitiwa walichaguliwa katika wilaya ya Micheweni na Mkoani. Katika wilaya ya Micheweni shehia ya Kwale na shehia ya Kiuyu Mbuyuni ndizo zilizotumika. Wilaya ya Mkoani walengwa walipatikana katika shehia za Mwambe na Chokocho. Wazee, watu wamakamo na vijana walihusishwa ili kuthibitisha kuwa viangama vinatumika kwa watu wa rika zote . Kila shehia walisailiwa watu 20, jumla ya shehia zote walisailiwa watu 80 . Kigezo cha wazee ni kuanzia miaka 60 na kuendelea, watu wa makamo kuanzia miaka 40 hadi 59 na vijana ni umri kati ya miaka 18 hadi 35. Walengwa hawa waligawiwa katika makundi matatu ili lengo la utafiti huu liweze kufikiwa kiurahisi, makundi hayo ni kundi la wageni waliokaa muda mrefu kisiwani Pemba, wageni waliokuja karibuni na wenyeji wa Pemba. Kundila kwanza lilijumuisha.

Watu 15 ambao ni wageni waliokaa muda mrefu kisiwani pemba aidha kundi la pili lilijumuisha wageni 15 waliokuja hivi karibuni kisiwani na kundi la tatu ni lilijumuisha watu 50 ambao ni wenyeji wa Pemba.

## 3.4 Mbinu za Ukusanyaji Data

Utafiti huu umetumia mbinu ya uwandani na mbinu ya maktabani.

### 3.4.1 Mbinu ya Uwandani

Kothari (1990) na Dawson (2002) wameeleza mbinu za ukusanyaji data kuwa ni zana au njia atakazotumia mtafiti katika ukusanyaji data.Utafiti huu ulifanyika uwandani katika kisiwa cha Pemba.Kama ambavyo Neuman (1991) aivyosema kuwa mkabala wa uwandani hutumika kukusanya data kutoka kwa watafitiwa wengi kwa kutumia mbinu za hojaji, usaili na ushuhudiaji.

Mkabala wa uwandani ni mzuri katika kukusanya data nyingi ili kufanya majumuisho ya matokeo, mawazo na kueleza uhalisia uliopo (Cohen na wenzake, 2000). Mtafiti alitumia mbinu za mahojiano, ushuhudiaji na hojaji ambazo zilimuwezesha kupata data zilizohusika na utafiti kutoka kwa sampuli lengwa. Mtafiti aliweza kufanyamajumuisho kutokana na data hizo. Mtafiti alitumia njia hizi kwasababuzilimwezeshakupata data zilizosadifu katika utafiti wake.

### 3.4.2 Mbinu ya Maktabani

Mbinu hii imetumiwa na mtafiti kwa madhumuni ya kuangalia machapisho mbalimbali kama vile vitabu, majarida, tasnifu na mitandao ili kuangalia nini kimeandikwa kuhusiana na mfumo angami katika lugha ya kiswahili. Maktaba

zilizotumika hapa ni maktaba ya Chuo Kikuu Huria tawi la Pemba pamoja na maktaba ya Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (TATAKI).

### 3.5 Njia za Ukusanyaji Data

#### 3.5.1 Usaili

Miongoni mwa mbinu zilizotumika kukusanyia data ni mbinu ya mahojiano. Kama ambavyo Enon (1998) alifasili mahojiano kuwa ni mbinu ya kuuliza maswali ya ana kwa ana, simu au barua pepe kati ya watu wawili au zaidi kwa lengo la kukusanya taarifa au maoni kuhusu swali la utafiti lililoainishwa.Katika utafiti huu mahojiano ya ana kwa ana yalitumika kwa sababu watoa taarifa walipatikana kwa urahisi. Njia hii ilimuwezesha mtafiti kuuliza maswali ya ziada, kupata nafasi ya kukutana ana kwa ana na watafitiwa, pia njia hii ilimsaidia mtafitiwa kupata ufafanuzi juu ya maswali asiyoyaelewa.

Hata hivyo mtafiti aliweza kukabiliana na changamoto kama vile watafitiwa kutotoa ushirikiano mzuri au kutokuwa tayari kuhojiwa.Mtafiti alifanya mahojiano na walengwakatika shuguli zao tofauti zikiwemo za kielimu, uvuvi na biashara .

#### 3.5.2 Ushuhudiaji

Kwa mujibu wa Enon (1998) ushuhudiaji ni kuhudhuria na kuwepo pale tukio linapotendeka na kukusanya taarifa zake. Baradyana na Ame (2007) wanasema, ushuhudiaji ni kitendo cha kuchunguza watafitiwa wanafanya nini badala ya kuwauliza maswali.

Kwa msingi huo njia hii huepusha athari za mtafiti kwa watoa taarifa kama vile, watoa taarifa kufuata namna ya utumiaji wa lugha wa mtafiti au mtoa taarifa kutoamajibu ya haraka juu ya alichoulizwa na mtafiti bila ya kutafakari kwa kina kwa hofu yakuonekana hajui. Njia hii inasaidia kupata data halisi kwani, wakati data za utafiti zinapokusanywa wazungumzaji wanakuwa wanaendelea na shughuli zao za kawaida bilawoga na wasiwasi wa aina yoyote ile kwa vile ukusanyaji wa data hufanyika bila ya wao wenyewe kujua. Pianjia hii inasaidia kupata data ambazo sio rahisi kupatikana kwa njia ya hojaji au majadiliano. Hivyo basi  mtafiti alijumuika katika mikusanyiko mbali mbali ya watu na kukusanya data kwa kusikiliza mazungumzo yao, data zilizokusanywa ziliweza kuainisha mfumo angami katika lahaja ya Ki pemba na  kueleza ni kwa kiasi gani viangama vinazuia mawasiliano fanisi kwa wageni wa lahaja ya Kipemba.

### 3.5.3 Hojaji

Enon (1998) anafasili hojaji kuwa ni mbinu inayotumia maswali yaliyoandikwa na mtafiti ili watafitiwa watoe majibu. Katika utafiti huu hojaji ziligawiwa kwa watafitiwa 24 ambao waliweza kusoma na kuandika. Mtafiti alipita katika sehemu mbali mbali kama  katika taasisi za elimu kugawa hojaji  kwa lengo la kupata data zinazoainisha  viangama tofauti  katika lahaja ya kipemba. Mtafiti alitumia njia hii kwa kupata data kutoka kwa  wazungumzaji wa Kiswahili kwani viangama hujitokeza zaidi katika mazungumzo.

## 3.6 Watoa Taarifa

Watoa taarifa ni watu muhimu katika utafiti wowote wa uwandani (Ismail 2010). Watoa taarifa walikaohusika katika utafiti huu ni watu themanini (80) kati ya hao

ishirini walitoka katika shehia ya Chokocho na wengine ishirini (20) walitoka katika shehia ya Mwambe ikiwa kutoka mkoa wa kusini Pemba. Kwa upande wa Mkoa wa Kaskazini Pemba watu ishirini (20) walitoka katika shehia ya Kiuyu Mbuyuni na wengine ishirini (20) walitoka katika shehia ya Kwale kama inavyoonekana katika jedwali lifuatalo:

**Jedweai Na.3.1. Idadi ya Watoa Taarifa**

| **WATOA TAARIFA** | **CHOKOCHO** | | **MWAMBE** | | **KWALE** | | **KIUYU MBUYUNI** | | **JUMLA** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | W’ke | W’me | W’ke | W’me | W’ke | W’me | W’ke | W’me | |
| Vijana | 03 | 04 | 03 | 04 | 03 | 04 | 03 | 04 | 28 |
| Wazee wa makamo | 03 | 04 | 03 | 04 | 03 | 04 | 03 | 04 | 28 |
| Wazee Wakongwe | 03 | 03 | 03 | 03 | 03 | 03 | 03 | 03 | 24 |
| Jumla kuu | 09 | 11 | 09 | 11 | 09 | 11 | 09 | 11 | 80 |

**Chanzo: Data kutokana na Mtafiti**

### 3.7 Uchambuzi wa Data

Uchambuzi unahusiana na utoaji waruwaza mbali mbali ili kuweza kuchunguza, kufafanua na hatimaye kutoa hitimisho kuhusu kipengele kinachochunguzwa (Silverman 2005).Data zilizopatikana katika utafiti zilichambuliwa kwa mkabala usio wa kiidadi. Walliman (20011) anaeleza kuwa,mkabala usio wa kiidadi ni mkabala wa

uchambuzi wa data kwa kuegemea zaidi katika maelezo, maoni, hisia na kadhalika kinyume na kufanya uchambuzi wa kitakwimu. Mkabala huu umemuwezesha mtafiti kutoa maelezo ya kina yanayofafanua mfumo wa maneno yenye viangama na jinsi yanavyozuia mawasiliano fanisi kwa wageni wa lahaja ya Kipemba yatajitokeza katika usaili na kwenye mazungumzo ya ana kwa ana. Jambo ambalo ndio shabaha kuu ya utafiti huu. Mtafiti alichambua viangama na athari zake kwa wageni wa lahaja ya Kipemba kwa kuzingatia malengo ya utafiti. Hata hivyo majadweli kadhaa pia yalitumika  katika utafiti huu kwa madhumuni ya kumrahisishia msomaji kuelewa kwa haraka na kwa wepesi zaidi.

### 3.8 Maadili ya Utafiti

Maadili ya utafiti ni yale matumizi ya kanuni adilifu ya utafiti wa kisayansi.Mtafiti katika utafiti wake aLIzingatia mambo yafuatayo:

Kwanza aLIomba ridhaa ya wenyeji kufanya utafiti wake kama vile barua ya sheha wa shehia aalizokwendakufanya utafiti wake. Pia aliwaarifu walengwa wake wa utafiti kuhusu utafiti wenyewe ambao ni viangama, hii ni kwasababu mada hii bado ni ngeni kwa watu wengi.

### 3.9 Hitimisho

Katika sura hii mtafiti amebainisha hatua, njia na mbinu mbalimbali zilizotumika katika ukusanyaji na uchambuzi wa data za utafiti huu. Vipengele vilivyoelezwa ni eneo la utafiti, walengwa wa utafiti, usampulishaji, mbinu za ukusanyaji data na uchambuzi wa data , maadili ya utafiti na mchakato wa utafiti.

# SURA YA NNE

# UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA

## 4.1 Utangulizi

Sura hii imeshughulikia uwasilishaji na uchambuzi wa data. Sura hii imegawanywa katika sehemu mbili. Sehemu ya kwanza inazungumzia mfumo angami katika Kiswahili cha Kipemba na sehemu ya pili inazungumzia ni kwa vipi mfumo angami wa Kipemba unakwamisha mawasiliano fanisi kwa wageni wa lahaja ya Kipemba.

## 4.2 Mfumo Angami wa Kiswahili cha Kipemba

Kama ilivyokwishaelezwa kuwa katika lugha nyingi baadhi ya mofimu zina ugumu katika uchambuzi wake (Zwicky, 1977) , katika Katamba na Stonham (2006), Mofimu za aina hii zinajulikana kuwa ni viangama. Tumeshaeleza pia katika kiunzi cha nadharia kuwa tumetumia nadharia ya Zwicky ya viangami (1977) kama ilivyoboreshwa na Katamba na Stonham (2006). Kwa hivyo tunapojadili mfumo angami tunajadili aina zoto za viangami vilivyomo katika lahaja ya Kipemba. Viangama katika lahaja ya Kipemba kama zilivyo lugha nyengine zinajitokeza mwanzoni na mwisho. Uchambuzi wa data hizi unalijibu swali la kwanza linalohusu maumbo mbali mbali ya viangami katika kiswahili cha Kipemba. Utafiti umebaini kuwa kiswahili cha Kipemba kina maumbo ya aina mbalimbali ya viangama ambayo hujitokeza mwanzo wa neno, katikati ya neno na mwishoni mwa neno. Data hizi zimepatikana kwa njia ya usaili na ushuhudiaji.

### 4.2.1 Viangama Tamati Viwakilishi

Viwakilishi vimeelezwa na wataalamu tofauti na kila mmoja akiwa na idadi na aina zake.Katika utafiti huu tumeeleza aina za viwakilishi ambavyo ni viangama tamati

katika lahaja ya Kipemba. Kwa mujibu wa data iliyokusanywa kuna viangama tamati viwakilishi nafsi, viangama tamati viwakilishi vimilikishi na viangama tamati viwakilishiviulizi.

Uchambuzi wa data zifuatazo unaonyesha maumbo ya viangama tamati katika lahaja ya Kipemba. Utafiti umebaini kuwa wazee, watu wa makamo na vijana hutumia maumbo haya katika mazungumzo yao. Data hizi zimekusanywa kwa njia ya mahojiano na ushuhudiaji. Data zifuatazo zinadhihirisha maumbo ya viangama tamati viwakilishi nafsi:

**Data 6**

**KP**: Mi**ye** na weye tufungu swaumu mwezi mzima

**KS**: Mimi na wewe tumefunga swaumu mwezi mzima

**KP**: Mi**ye** nimamuahidi mwanangu akapasi tampa zawadi nzuri

**KS**: Mimi nimemuahudi mtoto wangu akifaulu nitampatia zawadi nzuri

**KP**: Su**ye** si wageni wenu

**KS**: Sisi sio wageni wenu

**KP**: Nyu**ye** wana wadugu hamruhusiwi kwenda kisimani

**KS**: Nyinyi watoto wadogo hamruhusiwi kwenda kisimani

**KP**: Viwe kende na mwana**we**?

**KS**: Jee ,Viwe kaenda na mtoto wake?

**KP**: Mami**ye** Juma hanaronga na**si** sasa

**KS**: Mama yake Juma haongei na sisi sasa hivi

**KP**: Akaja kuno hanajana**ye**

**KS**: Atakapokuja huko hatokuja na yeye

**KP**: Ali apouka kangilina**o** woti garini

**KS**: Ali alipoondoka ameingia na wao wote kwenye gari

Utafiti umebaini kuwa maumbo ya viangama tamati viwakilishi nafsi katika lahaja ya Kipemba ni **ye** na **si** ambavyo hujidhihirisha katika nafsi ya kwanza umoja na wingi, ya pili wingi na nafsi ya tatu umoja na wingi ambapo mzungumzaji huweka silabi mbadala katika silabi ya pili ya viwakilishi vya nafsi ambavyo ni **ye** kama zilivyojidhihirisha katika baadhi ya sentesi hapo juu. Wakati mwingine hutokea udondoshaji wa silabi na kuungwa na kiunganishi kwa kama inavyoonekana katika baadhi ya sentesi hapo juu. Viangama tamati viwakilishi, **si**, **nyi**, **ye** na **o** hujidhihirisha katika viwakilishi vya nafsi ya tatu umoja na wingi. Utafiti huu umebaini kuwa mfumo wa viangama tamati viwakilishi katilka lahaja ya Kipemba mara nyingi hudondosha silabi ya pili kuliko ya kwanza na kuungwa na neno lililo mbele yake. Pia wapo watafiti waliobainisha viangama hivi katika tafiti zao kama Said katika utafiti wake kuhusu viangama katika Kipemba (2011). Vilevile Lambert katika utafiti wake kuhusu lahaja za Kenya Kivumba, Chijovu, Kingare na Chi-Chifundi.

### 4.2.2 Viangama Tamati Vivumishi

Uchambuzi wa data zifuatazo unaendeleakuonyesha mfumo angami wa lahaja ya Kipemba ambapo mtafiti ameonesha viangama tamati vivumishi katika lahaja ya Kipemba. Utafiti umebaini kuwa wazee, watu wa makamo na vijana wa Kipemba hutumia zaidi maumbo haya wakati wa mazungumzo yao. Data zimekusanywa kwa njia ya mahojiano na ushuhudiaji. Viangama tamati vivumishi vimejitokeza katika aina tatu, nazo ni:

Viangama tamati vivumishi vimilikishi.

Viangama tamati vivumishi vya sifa

Viangama tamati vivumishi viulizi

#### 4.2.2.1 Viangama Tamati Vivumishi Vimilikishi

Viangama hivi hutokana na udondoshaji wa sauti mbili za kati kama data zinavyojidhihirisha hapo chini:

**Data7**

**KP**: Kanpigwa ni mwana**we** wa kumvyaa

**KS**: Amepigwa na mtoto wake aliyemzaa

**KP:** Fatuma kakoswa ni mume**we**

**KS**: Fatma amekosewa ni mume wake

**KP:** Yeye kanachuki na ahali**ye**

**KS**: Yeye ana chuki na ndugu yake

**KP:** Haji yuko mazikoni kwa babu**ye**

**KS**: Haji yuko mazikoni kwa babu yake

**KP**: Babi**ze** machano wavyaligwa kumi na mbili

**KS**: Babu zake machano wamezaliwa kumi na mbili

**KP**: Hende kwa ndugu**ze** kiasi

**KS:** Haendi kwa ndugu zake

Data za hapo juu zinaonyesha kuwa mfumo angami wa Kipemba una viangama **we**, **ye** na **ze** ambavyovimepatikanabaada ya kudondoshwa sauti mbili za kati ambazo ni

//ak// katika neno lililobeba kiangama, udondoshwaji huo unaonekana katika maneno yafuatayo:

**Data8**

| **Neno** | **Uangami** |
|---|---|
| Mwana w**ak**e | Mwana**we** |
| Mume w**ak**e | Mume**we** |
| Mjomba w**ak**e | mjomba**we** |
| Babu y**ak**e | Babu**ye** |
| Baba z**ak**e | Babi**ze** |
| Ndugu z**ak**e | Ndugu**ze** |

Vingama tamati  hivi huegemezwa kwenye maneno yenye maumbo ya umoja  kama neno **mjomba, babu, baba** na **nduguna** pia kwenye maneno yenye maumbo ya umoja na wingi kama maneno **mwana** na **mume** kama inavyoonekana katika tungo ya kwanza na ya pili hapo juu, vile vile viangama hivi husimama katika nafsi ya tatu umoja.

Pia vipo viangama **wo,yo,** na **zo** ambavyo hujitokeza katika maumbo mengine tofauti.  Kama inavyoonekana katika data zifuatayo:

**Data 9**

**KP**: Kunnda shamba na mke**wo**?

**KS**: Umekwenda shamba na mke wako?

**KP**: Mwana**wo** kapigwa jibwe na mwana wa jirani

**KS**: Mtoto wako amepigwa jiwe na mtoto wa jirani

**KP:** Zawadi zino zinarudi kwa mkwe**wo**

**KS**: Zawadi hizo zinatoka kwa mkwe wako

**KP:** Weye usimtume babi**yo** dukani

**KS**: Wewe usimtume baba yako dukani

**KP**: Kunakwitwa ni dadi**yo** leo

**KS**: Unaitwa ni dada yako leo

**KP**: Mami**yo** kakutwa ni tumbo la kuhara

**KS**: Mama yako anaumwa ni tumbo la kuharisha

**KP**: Jee, kutauka na ndugu**zo**?

**KS**: Jee, utaondoka na ndugu zako?

**KP**: Hili ni posho lya rafiki**zo**

**KS**: Hili ni posho la rafiki zako

Data zimeonesha kuwa kiangama tamati kivumushi kimilikishi **yo, wo** na **zo** ni viangama vilivyopatikana kutokana na udondoshaji wa silabi mbili za kati kama tulivyooneha katika data iliyotangulia nanma inavyobainisha udondoshaji wa sauti //ak//, viangama hivi huegemezwa katika nomino zenye maumbo tofauti. Kwa mfano katika sentensi ya (1-3) viangama vimeegemezwa katika nomino zenye maumbo ya umoja na wingi na vimesimama katika nafsi ya pili umoja. Pia viangama vilivyo katika sentensi ya (4-6) vimeegemezwa katika nomino za umoja tu na vimesimama katika nafsi ya pili umoja. Vilevile viangama vilivyomo katika sentensi ya (7-8) vimeegemezwa katika nomino za wingi na vimesimama katika nafsi ya pili umoja.

Kwa mujibu wa data zilizochambuliwa tumebaini kuwa mfumo angami tamati wa vivumishi vimilikishi katika lahaja ya Kipemba husimama katika nafsi ya pili umoja na pia nafsi ya tatu umoja. Uangami huu unahusisha ngeli zote za nomino. Mtafiti ameweka muhutasari wa jedwali  linalooonesha viangami vinavyojibandika kwenye nomino zilizotangulia vimilkishi vilivyopoteza baadhi ya vijenzi vyake.

**Jedwali Na:4.1 Viangama Vimilikikishi Nafsi ya Pili na ya Tatu Umoja**

| **Ngeli** | **Viangama Vimilkisha Nafsi ya Pili na ya Tatu** | | |
|---|---|---|---|
| | | **N2** | **N3** |
| ½ | **U** | ***-wo*** | ***-we*** |
| | **W** | ***-wo*** | ***-we*** |
| ¾ | **U** | ***-wo*** | ***-we*** |
| | **W** | ***-yo*** | ***-ye*** |
| **5/6** | **U** | ***-lo*** | ***-le*** |
| | **W** | ***-yo*** | ***-ye*** |
| **7/8** | **U** | ***-cho*** | ***-che*** |
| | **W** | ***-vyo*** | ***-vye*** |
| **9/10** | **U** | ***-yo*** | ***-ye*** |
| | **W** | ***-zo*** | ***-ze*** |
| **11/12** | **U** | ***-wo*** | ***-we*** |
| | **W** | ***-zo*** | ***-ze*** |
| **13/14** | **U** | ***-wo*** | ***-we*** |
| | **W** | ***-yo*** | ***-ye*** |
| **15** | **U** | ***-po*** | ***-pe*** |
| **16** | **U** | ***-ko*** | ***-kwe*** |
| **17** | **U** | ***-mo*** | ***-mwe*** |
| **18** | **U** | ***-ko*** | ***-kwe*** |

**Chanzo:Data kutoka  Uwandani (2018)**

i) Hapo chini mtafiti wa kazi hii ameonesha nomino za ngeli mbalimbali jinsi zilivyoangamishwa na viangama vimilikishi vilivyooneshwa kwenye jedwali (4.1 ) hapo juu:-

**Jedwali Na: 4.2 VivumishiVimilikisha vya Nafsi ya Pili**

| **Ngeli** | **Kipemba** | |
|---|---|---|
| | **U** | **W** |
| ½ | Nzee***wo*** | Wazee***wo*** |
| ¾ | Nti***wo*** | Miti***yo*** |
| **5/6** | Jiwe***lo*** | Mawe***yo*** |
| **7/8** | Kiti***kyo*** | **V**iti***vyo*** |
| **9/10** | Nguo***yo*** | Nguo***zo*** |
| **11/12** | Uzi***wo*** | Nyuzi***zo*** |
| **13/14** | Ugonjwa***wo*** | Magonjwa***yo*** |
| **15** | Kucheza***ko*** | - |
| **16** | Pahali***po*** | Mwahali***mo*** |
| **17** | Nyumbani***mo*** | Nyumbani***mo*** |
| **18** | Kwahal***iko*** | Kwahali***ko*** |

**Chanzo:Data kutoka Uwandani (2018)**

ii) **Vivumishi Vimilikishi vya Nafsi 3**

Hapo chini mtafiti wa kazi hii ameonesha nomino za ngeli mbalimbali jinsi zilivyoangamishwa na viangama vimilikishi vilivyooneshwa kwenye jedwali ( ) hapo juu:-

**Jedwali Na: 4.3 Vivumishi Vimilikisha vya Nafsi ya Tatu**

| **Ngeli** | **Kipemba** | |
|---|---|---|
| | **U** | **W** |
| ½ | Nzee***we*** | Wazee***we*** |
| ¾ | Nti***we*** | Miti***ye*** |
| **5/6** | Jiwe***le*** | Mawe***ye*** |
| **7/8** | Kiti***kye*** | **V**iti***vye*** |
| **9/10** | Nguo***ye*** | Nguo***ze*** |
| **11/12** | Uzi***we*** | Nyuzi***ze*** |
| **13/14** | Ugonjwa***we*** | Magonjwa***ye*** |
| **15** | Kucheza***kwe*** | - |
| **16** | Pahali***pe*** | Mwahali***mwe*** |
| **17** | Nyumbani***mwe*** | Nyumbani***mwe*** |
| **18** | Kwahali***kwe*** | Kwahali***kwe*** |

**Chanzo:Data kutoka Uwandani (2018**

iii) **Kivumishi Kimilikishi – *ngwa***

Waongeaji wa lahaja ya Kipemba hutumia kipashio '***ngwa'*** kubainisha umilikishi kwa mtu ambaye hakuainishwa wazi wazi. Mifano ifuatayo hapo chini inaonesha ukweli huu huku ikitafsiriwa kwa Kiswahili Sanifu

**Data 10**

**43.** (a) **KP:** *Mume**ngwa***

**KS:** *mume **wa watu***

(b) **KP:** *Mifenesi**ngwa***

**KS:** *Mifenesi **ya watu***

(c) **KP:** *Nchumba**ngwa***

**KS:** *Mchumba **wa watu***

(d) **KP:** *Ardhi**ngwa***

**KS:** *Ardhi **ya watu***

Katika mifano ya hapo chini kiangama ***–ngwa***kimeangama kwenye nomino inayobainisha umilikishi kwa mtu ambaye hakuainishwa wazi wazi.

### 4.2.2.2 Viangama Tamati Vivumishi vya Sifa

Viangama hivi hueleza sifa ya kitu na huegemezwa katika nomino. Data zifuatazo zinadhihirisha mfumo angami wa tamati wa vivumishi vya sifa katika lahaja ya Kipemba:

**Data 11**

**KP**: Mwalimu kavyalya saa**pya**

**KS:** Mwalimu amevaa saa mpya

**KP**: Juma kagele simu**pya** jana

**KS**: Juma amepoteza simu mpya jana

**KP:** Sikukuyu ino heweshonewa nguo**pya**

**KS:** Sikukuu hiyo hawakushonewa nguo mpya

**KP**: Babiye Makame kavunjiwa nyumba**pya**

**KS:** Babu yake makame amevunjiwa nyumba mpya

Data hizi zinaonesha kuwa kiangama tamati kivumishi cha sifa hupatikana kwa kudondosha sauti moja ya mwanzo nayo ni//m//katika neno mpya, na huegemezwa

katika nomino zenye umbo la umoja tu, mfano wa maneno yenyewe ni **“**saa, simu**,** na **“**nyumba” kama yanavyoonekana katika sentensi za hapo juu.

Vile vile kuna kiangama **to** ambacho hupatikana kwa kuwekwa kijinenombadala wa kielezi sana na huegemezwa katika kivumishi kilichopo kabla yake, kama data zinavyoonesha hapo chini.

**Data 12**

**KP**: Jibwe hilyo kulyu**to** (kubwa sana)

**KS**: Jiwe hilo kubwa sana

**KP**: Ino nyumba zuri**to**

**KS**: Hiyo nyumba nzuri sana

Baadaya kuangalia data zote hizi tumegundua kuwa viangama tamati vivumishi vya sifa havipatikani kwa njia ya udondoshaji tu bali pia kwa njia ya mbadala wa vijineno fulani.

### 4.2.2.3 Viangama Tamati Vivumishi Viulizi

Katika lahaja ya Kipemba viangama tamati vivumishi viulizi ni **na** na **nga** ambavyo hupatikana kwa kudondoshwa silabi ya mwisho katika neno husika, na hutumika kuuliza maswali ya nani na ngapi. Data zifuatazo zinadhihirisha hayo:-

**Data 13**

**KP**: Asha kavyalya wana we**nga?**

**KS:** Asha amezaa watoto wangapi?

**KP**: Mwanawe ataja sa**nga?**

**KS:** Mtoto wake atakuja saa ngapi?

**KP**: Babiyo kalya machungwa me**nga?**

**KS:** Babu yako amekula machungwa mangapi?

**KP**: Yano matambara ya**na?**

**KS:** Yale matambara yana nini?

**KP:** Lino paka jizi lya**na?**

**KS:** Lile paka jizi la nani?

**KP**: Lelwo kuja na**na?**

**KS**: Leo umekuja na nani?

### 4.2.3 Viangama Tamati Vielezi

Uchambuzi wa data zifuatazo unaendelea kutuonesha mfumo angami wa lahaja ya Kipemba. Maumbo ya viangama tamati vielezi yanaonekana kutumiwa kwa wingi katika mazungumzo ya kila, utafiti utaumeonesha kuwa wazee, watu wa makamo na vijana wanatumia maumbo ya viangama hivi zaidi katika mazungumzo yao. Data hizi zimekusanywa uwandani kwa njia ya mahojiano na ushuhudiaji.

Utafiti umeonesha kuwa kuna vielezi ambavyo vinaweza kutumiwa kama viangama tamati katika lahaja ya Kipemba vimejigawa katika aina tatu, aina zenyewe ni:

Viangama tamati vielezi vya pahala

Viangama tamati vielezi vya namna au jinsi

Viangama tamati vielezi vya idadi au kiasi

**(a) Viangama tamati vielezi vya pahala**

Viangama hivi hupatikana kwa kudondoshwa silabi ya kwanza na vingine hudondshwa silabi ya pili katika neno, data zifuatazo zinafafanua aina hii ya viangama.

**Data 14**

i) **KP:** Viatu vyakwe kavigelya**ko** jayani.

**KS:** Viatu vyake amevitupa huko jaani

ii) **KP:** Mwana kalyalya**ko** nyumbani.

**KS:** Mtoto amelala huko nyumbani

iii) **KP:** Uno mkanda huvaligwa**po** kiunoni.

**KS**: Huo mkanda huvaliwa hapo kiunoni

iv) **KP**: Kende**po** dukani

**KS**: Kaenda hapo dukani

v) **KP**: Panya mdugu kanacheza**mo** nyumbani.

**KS**: Panya mdogo anacheza humo nyumbani

vi) **KP:** Kake kakitili**mo** mkobani mwakwe.

**KS**: Kaka kakitia humo mkobani mwake

vii) **KP**: Kamkutu dadiye kajinamili**chi**chumbanimwe

**KS**: kamkuta dada yake kajiinamia chini chumbanimwe

viii) **KP:** Wanafuzi woti wamakaya**chi** darasani

**KS**: Wanafunzi wote wanakaa chini darasani

ix) **KP**: Mgeni wetu kende**wa**?

**KS**: Mgeni wetu amekwenda wapi?

x) **KP**: Posho lyako nikutilile**wa**?

**KS**: Posho lako nikutilie wapi?

Kwa mujibu wa data za hapo juu, viangama tamati **ko**, **po** , **mo** na **chi** katika sentensi ya (i-viii) hutumika kuonesha pahala gani tendo limefanyika, na vinatokana na udondoshaji wa silabi. Kiangama **ko** na **mo v**inatokana naudondoshaji wa silabi ya kwanza $hu$ katika neno huko na humo. Kiangama **po** kinatokana na udondoshaji wa silabi ya kwanza $ha$ katika neno hapo. Na kiangama **chi** kinatokana na udondoshaji wa silabi ya pili $ni$ katika neno chini.

Data zinaendelea kuonesha kuwa kiangama tamati **wa** hutumika kuulizia maswali yenye kutaka kujua wapi tendo limetendeka. Kiangama **wa** kinatokana na udondoshaji wa silabi ya pili $pi$ katika neno *wapi*. Kiangama **wa** huungwa mwishoni mwa neno lililo nyuma yake kwa hiyo ni kiangama tamati kama data zilivyodhihirisha hilo hapo juu. Ifahamike hapa kuwa upo uwezekano wa kutumia neno *wapi* kama neno linalojitegemea. Hii husababishwa na muundo wa sentensi iliyotumika. Mfano katika sentensi zifuatazo:

**Data 15**

a) **KP:** Wanafunzi woti wende *wapi* juzi?

**KS:** Wanafunzi wote walikwenda wapi juzi?

b) **KP:** Yule mgeni kalekele *wapi* leo?

**KS:** Yule mgeni ameelekea wapi leo?

c) **KP**: Umalyalya *wapi* jana?

**KS**: Umelala wapi jana?

d) **KP**: Yuno mbuzi kanalilia *wapi* leo?

**KS**: Huyo mbuzi analilia wapi leo?

e) **KP**: Mwna mdogo kawa *wapi* jana?

**KS**: Mtoto mdogo alikuwa wapi jana?

Data zinaonesha kuwa kiangama kinachotumika badala ya neno *wap*i pia kimeelezewa na wataalamu kama vile Polome alitumia kiangama **pi** lakini katika Kipemba hutumika kiangama **wa** badala ya kiangama **pi** kama data zinavyojidhihirisha hapa chini:-

**Data 16**

**i.** **KP:** Uno mkoba kununuu**wa?**

**KS:** Huo mkoba umeununua wapi?

**ii.** **KP**: Ubwabwa wa maulidi upikiwa**wa?**

**KS**: Wali wa maulidi umepikiwa wapi?

iii. **KP**: Kisucho kipotelea**wa**?

**KS**: Kisu chako kimepotelea wapi?

iv. **KP**: Mgeniwo kumwono**wa**?

**KS**: Mgeni wako umemuona wapi?

v. **KP**: Vyombovyo viokotewa**wa**?

**KS**: Vyombo vyako vimeokotwa wpi?

Data zinaonesha kuwa kiangama tamati kiulizi **wa** huungwa kwenye kitenzi na hakiwezi kuungwa katika kategoria nyingine za maneno kwani huenda sambamba na vitenzi.

(b) **Viangama Tmati Vielezi vya Namna au Jinsi**

Viangama hivi ni **to**, **taa** na **je** ambavyo havitokani na udondoshaji bali ni mofimu maalumu ambayo kimatamshi hutamkwa pamoja na neno lililo nyuma yake kama data zinavyodhihirisha hilo:

**Data 17**

a) Kamgojo**taa** hela hechomoza

Alimsubiri sana lakini hakuchomoza

b) Mwana huyu kafyaka**taa** usiku

Mtoto huyu alihangaika sana usiku

c) Yeye hanamuheshimu**taa** kakiye

Yeye hamuheshimu hata kaka yake

**d)** Jana tupouka mjini tuchoko**to**

Jana tulipoondoka mjini tulichoka sana

e) Mheshimiwa wetu kaseme**to** mkutanoni

Mheshimiwa wetu amesema sana mkutanoni

f) Mwana ayelia katende**je**?

Mtoto anayelia amefanya nini?

g) Umefanya**je**?

Umefanya nini?

Data zinaonyesha kuwa viangama **to** na **taa** ni viangama tamati vielezi vinavyoeleza utendekaji wa jambo kwa muda mrefu, na **je** ni kiangama kinachoeleza namna ya utendekaji wa jambo. Kwa hivyo viangama hivi katika lahaja ya Kipemba

ni viangama tamati vielezi kwa sababu vinafanya kazi ya kuelezea vitenzi katika sentensi hizo.

### (c) Viangama tamati Vielezi vya Idadi au Kiasi

Kiangama hiki ni **nga** ambacho hupatikana kwa njia ya udondoshaji wa mofimu fulani katika neno husika na hugandamizwa katika kitenzi na hujitokeza katika hali ya kuuliza, kama mifano inavyoonekana hapo chini.

**Data 18**

i) **KP**: Zino pesa kukwa**nga**?

**KS**: Hizo pesa zilikuwa ngapi?

ii) **KP**: Mno mkobanimwe katili**nga**?

**KS:** Humo mkobani mwake katia ngapi?

iii) **KP**: Kino kitoto nicha**nga**?

**KS**: Hicho kitoto ni changapi?

iv) **KP**: Hiko kikao kitaja saa**nga**?

**KS**: Hicho kikao kitakuwa saa ngapi?

v) **KP**: Zino mbegu ziwa**nga**?

**KS**: Hizo mbegu zilikuwa ngapi?

Kwa hivyo viangama hivi katika lahaja ya kipemba ni viangama tamati vielezi kwa sababu vinafanya kazi ya kielezi katika mazingira hayo

### 4.2.3 Viangama Tamati Viunganishi

Uchambuzi wa data zifuatazo unaendelea kuonyesha mfumo angami wa lahaja ya Kipemba kwa kuangalia maumbo ya viangami tamati viunganishi. Utafiti umeonyesha kuwa wazee, watu wa makamo na vijana hutumia viangama hivyo katika mazungumzo yao ya kila siku. Data hizi zimepatikana uwandani kwa njia ya mahojiano na ushuhudiaji. Kwa mujibu wa data iliyokusanywa kiangama hiki hakipatikani kwa kudondosha bali hutumia mofimu mbadala wa neno kama data zinavyodhihirisha hapa chini:

**Data 19**

i) **KP**: Sijamwona pano yapata**ja** miezi miwili

**KS:** Sijamuona hapa inafika kama miezi miwili

ii) **KP**: Kanaronga**ja** mwana mdugu

**KS**: Anaongea kama mtoto mdogo

iii) **KP**: Kanazurura**ja** mwana msi na kwao

**KS**: Anazurura kama mtoto asiye na kwao

iv) **KP**: Kanakunywa maji**ja** gari bovu

**KS**: Anakunywa maji kama gari bovu

v) **KP**: Babiye somo mnene**ja** mbuyu

**KS**: Babu yake somo ni mnene kama mbuyu

Kutokana na data hizo, utafiti umebaini kuwa kiangama **ja** ni mbadala wa neno **kama** nahuungwa kwenye vitenzi na kwenye nomino na hufanya kazi ya

kiunganishi. Ufafanuzi huo umeonyesha kuwa kiangama **ja** kinapoungwa kwenye nomino huwa kiunganishi na kinapoungwa kwenye kitenzi huwa kielezi.

### 4.2.4 Viangama Tamati Vitenzi

Uchambuzi unaendelea kufafanua mfumo angami wa Kipemba, hapa tunafafanua viangama tamati vitenzi katika lahaja ya Kipemba,viangama tamati vitenzi hujitokeza katika mfumo angami wa lahaja ya Kipemba. Maumbo ya viangamatamati vitenzi katikalahaja ya Kipemba yanayojitokeza katika mfumo huo ni haya yafuatayo:

**Data 20:**

i) **KP**: Natake**nda** shamba kesho

**KS**: Ninataka kwenda shamba kesho

ii) **KP**: Wantake**nda** ng'ambu?

**KS**: Wanataka kwenda kijijini

iii) **KP**: Yuno mwana hantake**nda** chuoni

**KS**: Yule mtoto hataki kwenda chuoni

iv) **KP**: Kantake**nda** nyumbani sasa

**KS**: Anataka kwenda nyumbani

v) **KP**: Ndo**nda** shamba

**KS**: Ndio ninaenda shamba

Data hizi zinafafanua maumbo ya viangama tamati vitenzi, katika lahaja ya Kipemba ambapo data hizi zinatupa kiangama **nda** kilichomo ndani ya kitenzi kikuu ambacho kimeegemezwa katika vitenzi visaidizi baada ya kudondoshwa silabi ya kwanza

$kwe$ ya kitenzi kikuu *kwenda* kama inavyojidhihirisha katika sentensi ya (i-iv) hapo juu.

Katika sentensi ya (v) pamejitokeza kiangama **nda** ambachokimepatikana baada ya kudondoshwa silabi tatu za mwanzo katika kitenzi kikuu. Vile vile kuna maumbo mengine ya viangama tamati vitenzi kama yanavyo jidhihirisha katika data zifuatazo:

**Data21**

| | | |
|---|---|---|
| **i)** | **KP**: | Mgonjawe pandu kesha**fa** |
| | **KS**: | Mgonjwa wake Pandu keshakufa |
| **ii)** | **KP**: | Mwanao kesha**nya** |
| | **KS**: | Mtoto wako keshakunya |
| iii) | **KP**: | Wageni wamaofika wesha**lya** choti |
| | **KS**: | Wageni waliofika weshakula chote |
| iv) | **KP**: | Asha kesha**ja** nyumbani |
| | **KS**: | Asha ameshakuja nyumbani |
| v) | **KP**: | Mwanawe kesha**wa** mkubwa |
| | **KS**: | Mtoto wake keshakuwa mkubwa |

Data zinaendelea kubainisha kuwa katika mfumo angami wa Kipemba kuna maumbo tofauti tofauti katika viangama tamati vitenzi,data zinaonesha kuwa mfumo angami wa Kipemba wa viangami tamati vitenzi hupatikana baada ya udondoshwaji wa silabi ya kwanza katika kitenzi kikuu na kuwa kitenzi kisaidizi. Viangama **fa**, **nya**, **wa**, **ja** na **lya** vimepatikana baada ya kudondoshwa silabi $ku$ katika kitenzi kikuu, kama inavyojioonesha hapo juu.

Kwa ujumla data zimechambuliwa na zimelijibu swali la msingi kuhusu mfumo angami wa lahaja ya Kipemba.  hivyo utafiti umegundua kuwa mfumo angami wa lahaja ya Kipemba unajidhihirisha mwanzoni mwa neno na mwishoni mwa maneno kama ambavyo vinavyoonekana wazi katika jadweli lifuatalo.

Jedwali Na.4.4 Viangama tamati katika lahaja ya Kipemba.

**Jedwali Na: 4.4 Muhutasari wa Maumbo ya Viangama Mbalimbali**

| **Viangama tamati viwakilishi** | **Viangama tamati vielezi** | **Viangama tamati viunganishi** | **Viangama tamati vitenzi** |
|---|---|---|---|
| *-ye,-si,-o,-we,-ze,-zo,-wo,-yo,-pya,-to,-nga,-na.* | *-ko,-po,-mo,-chi,-wa,-to,-taa,-je,-nga.* | *-ja.* | *-nda,-ja,-nya,-wa,-lya.* |

**Chanzo: Data kutoka Uwandani (2018)**

## 4.3 Mfumo Angami Jinsi unavyokwamisha Mawasiliano Fanisi

Mfumo angami wa Kipemba unatumiwa na Wapemba katika mawasiliano yao ya kila siku.Mfumo huu ni kikwazo kikubwa kwa wageni wa lahaja hii ya Kipemba ambao kwa njia moja au nyengine huamiliana nawatumiaji wa lahaja hii ya Kipemba. Mara nyenginemfumo angamihusababisha kutokea kutofahamiana katika mawasiliano baina ya Wapemba na wagenii wa lahaja ya Kipemba.

Baada ya kuonesha mfumo angami wa lahaja ya Kipemba hapa tunajibu swali la pili la msingi katika utafiti huu ambalo ni kwa namna gani mfumo angami wa lahaja ya Kipemba unakwamisha mawasiliano kwa wageni wa lahaja hio. Kipengele hiki

kinaonesha athari za kimawasiliano zinazowapata wageni wa lahaja ya Kipemba hasa kutokana na mfumo angami wa lahaja hio.

Utafiti huu ulteuwa jibu la *ndiyo* au *hapana* ili kupima kiwango cha tatizo la kukwama mawasiliano fanisi kati ya wenyeji wanaotumia mfumo angami na wageni wasiouelewa mfumo angami wa Kipemba. Swali hilo liliuliza kwamba, je? kuna tatizo lolote la kimawasiliano linaloweza kujitokeza wakati mzungumzaji wa Kipemba anapozungumza na msikilizajiambae ni mgeni wa lahaja hio. Utafiti huu umeonesha kuwa kati ya watafitiwa 80 waliojibu dodoso, watafitiwa 68 kati ya waliohojiwa sawa na asilimia (85%) walikubali kuwa mfumo angami wa Kipemba huleta tatizo la kimawasilino kwa wageni wa lahaja ya Kipembaambapo watafitiwa 08 kati ya themanini waliohojiwa sawa na asilimia (10%) walikataa kuwa mfumo angami wa Kipemba huleta tatizo la kimawasiliano kwa wageni wa lahaja ya Kipemba na watafitiwa wa nne4 sawa na asilimia(05%)walisema hawajui na kwa hivyowaliacha wazi sehemu za kujibia bila kujaza neno *ndiyo* au *hapana.* Kwa hiyo utafiti unaonesha kwamba watafitiwa wengi walisema ndiyo yaani mfumo angami wa lahaja ya Kipemba unaleta tatizo la kimawasiliano kwa wageni wa lahaja hio. Idadi hiyo ilikuwa kubwa zaidikuliko ya wale waliokataa.

Aidha utafiti huu ulitaka kujua aina ya matatizo yaliyojitokeza kutokana na matumizi ya mfumo angami wa lahaja ya Kipemba kwa wageni wa lahaja hio. Utafiti ulibaini kuwa mfumo angami wa lahaja ya Kipemba husababisha matatizo kadhaa yakiwemo kutokufahamiana katika mazungumzo, husababisha migogoro katika jamii, kuigawa jamii, kupoteza muda na kusababisha ufahamu mbaya wa kile kilichokusudiwa. Jedwali 4.5 Linaonyesha matatizo ya kimawasiliano yanayojitokeza kutokana na

matumizi ya mfumo angami wa lahaja ya Kipemba kwa wageni wa lahaja ya Kipemba.

### 4.3.1 Kutofahamiana katika Mazungumzo

Jibu hili limejitokeza mara sita (06) miongoni mwa watafitiwa ishirini na nne waliohojiwa. Mifano iliyotolewa inayoweza kusababisha kutokuelewana ni mingi. Hapa mtafiti amechaguwa mitatu na kuieleza kama alivvyodokezwa na wahojiwa.

*Kanfiwa* ***ndadaye.*** 'Ndadaye'ni kifungu cha maneno kilichojengwa na maneno matatu**. *Ni dada yake. Ni*** *imepoteza irabu yake* ***'i'*** na yake imepoteza kijenzi chake ***'-ak--'*** **.** Vijisehemu vya maneno vilivyobaki yaani **'n'** na **'–ye-** vimeambikwa kwenye nomino 'dada' na hivyo kujenga kitu kinachoonekana kama neno moja **n**dada**ye** lisilo maana iwapo litachukuliwa kama leksimu moja. Mgeni wa lugha aliyejifunza Kiswahili au hata muongeaji wa Kiswahili Sanifu asiyekuwa Mpemba au asiyekizowea Kipemba hawezi kuelewa kilichokusudiwa kimaandishi wala kimatamshi. Kwa msingi huu kufahamiana kutakosekana.

Sentensi nyengine ni ile isemayo kwamba"Mwana**o** kesha**nya".** Hapa pana viangama viwili; cha kwanza ni **'o'** kilichoambikwa kwenye neno '**mwana**' na cha pili ni '**nya'** kilichoambikwa kwenye neno **'kesha'. Kiangama 'o'** kimenyokolewa kutoka kwenye neno **wako** lililopoteza kijenzichake **'-ako-'.** Mgeni wa lugha anaweza kudhani kwamba neno 'keshanya' ni moja, lakini kwa kweli siyo hivyo. Ni neno moja lililobandikwa kiangama mwishoni mwake. Neno mwana**o** pia linaonekana ni moja lakini ukweli ni neno moja lenye kiangama mwishoni. Kesha**nya** kama leksimu halina maana na mwana**o** kama leksimu haina maana. Hivyo kwa asiyejua Kipemba

au asiyeelewa michakato ya kisarufi atakosa mawasiliano fanisi. Sentensi isemayo ka**n**potea na mtumbwi**we**litamlazimisha msikilizaji aulize maana ya **‘**mtumbwi**we’**. Jambo ambalo litakwamisha mawasiliano fanisi”.Kwa ujumla tunaweza kusema kuwa baadhi ya sentensi angami hazieleweki na hivyo kuleta tatizo la kimawasiliano baina ya wanyeji na wageni wa lahaja ya Kipemba, tatizo hili linasababishwa na mfumo angami wa lahaja ya Kipemba hasa kwa vile mfumo angami wa Kipemba una tabia ya udondoshaji wa silabi katika maneno yanayopachikwa viangama.

### 4.3.2 Kuigawa Jamii na Kupoteza Muda

Vilevile mtafiti ameona kwamba sentensi zenye mfumo angami wa lahaja ya Kipemba unasababisha kupotea kwa muda kutokana na kuwa wageni wa lahaja ya Kipemba hawaelewi kile kilichokusudiwa hivyo wageni hawa huchukua muda mrefu zaidi ili kujaribu kutafakari na kutafsiri maana halisi ya kile kilichokusudiwa. Mwisho tunaona kuwa mfumo angami wa lahaja ya Kipemba husababisha kutokea kwa ufahamu mbaya kwa wageni wa lahaja ya Kipemba.

Mzee mmoja aitwae Makame Haji Foum aliyehojiwa siku ya tarehe 25/05/2018 alipoulizwa ni mgawanyiko gani huweza kujitokeza? Alitoa jibu kwa kusema “Wapemba wanaotumia viangama huweza kusababisha mgawanyiko kati yao na wageni wao. Wapemba hueleweka kama kwamba wanaongea lugha nyengine kinyume na Kiswahili. Kwa msingi huo wao wanaweza kuhesabiwa kwamba wao ni watu wa jamii lugha moja na wageni wao ni watu wa jamii lugha nyengine”. Huo ni aina ya mgawanyiko unaojitokeza. Mzee alisisitiza.Asipofahamu maana iliyokusudiwa msikilizaji atahitaji maana ya kiufafanuzi wa lugha angami. Jambo hili la kutaka ufafanuzi litasababisha muda mwingi kupotea bure. Kwa hivyo tunaweza

kusema kwamba mfumo angami unaweza kusababisha upotevu wa muda na kuleta mgawnyiko.

### 4.3.3 Ufahamu Mbaya na Kujengeka Migogoro

Baadhi ya maneno hujidhihirisha kama siyo maneno ya Kiswahili na hujengeka katika mtizamo wa msamiati mpya.Wageni wanaposhindwa kuelewa hujiona kama wamebabaishwa ili wasiupate ujumbe. Watu hawa hukasirika na kuingiza roho mbaya ndani ya myoyo yao, hivyo kwa kiasi fulani hujenga chuki isiyo ya lazima. Hii ni aina fulani ya mgogoro.Baadhi ya sentensi huonyesha wazi kuwa kuna ugumu mkubwa wa masiliano kwa wageni wa lahaja ya Kipemba ambapo ugumu huu husababisha kutoke kwa kwa migogoro katika jamii kwani baadhi ya sentensi hizi huonekana kama ni matusi kwa wageni wa lahaja ya Kipemba mfano mzuri ni sentensi nambari tisa " Wenda kwa mami**yo** na babi**yo** ukawafise kisiwani.

**Jedwali Na: 4.5 Pingamizi zinazojitokeza katika Mfumo Angami wa Kipemba**

| **Idadi ya Uradidi** | **Aina ya Pingamizi** |
|---|---|
| **Mara 6** | Husababisha migogoro katika jamiii |
| **Mara 6** | Kutokufahamiana katika mazungumzo |
| **Mara 5** | Kuigawa jamii |
| **Mara 5** | Kupoteza muda |
| **Mara 2** | Husababisha ufahamu mbaya |
| **24** | |

**Chanzo:Data kutoka Uwandani**

Sentensi zifuatazo zinaonesha matatizo ya kimawasiliano yaliooneshwa na baadhi ya watafitiwa:

**Data 22**

i) **KP**: Kancheka**taa** hemwemuona

**KS**: Amecheka sana hamkumuona

**ii)** **KP**: Kanchinjwa nkisu**che** chumbani**mwe**

**KS**: Amechinjwa na kisu chake chumbani mwake

iii) **KP**: Mjomba**we** ka**n**pigwa nngombe**we**

**KS:** Mjomba wake amepigwa na ngombe wake

iv) **KP**: Pesa**ze** Juma z**e**vuja mfukoni**mwe**

**KS**: Psa zake Juma zilivuja mfukoni mwake

v) **KP**: Babi**ye** Ali endaja mwanamdogo

**KS**: Baba yake Ali anakwenda kama mtoto mdogo

**vi)** **KP**: Fatuma hepata**ta**shanuo kwa ndugu**ze**

**KS**: Fatma hakupata hata shanuo kwa ndugu zake

**vii) KP**: Mno mkobani**mwe** katili**nga?**

**KS**: Humo mkobani mwake katia ngapi?

**Vii) KP**: Mwana anolia katnda**je**?

**KS**: Mtoto anaelia amefanyaje?

**viii)KP**: Wenda kwa mami**yo** na babi**yo** ukawafise kisiwani

**KS**: Nenda kwa mama yako na baba yako ukawapeleke kisiwani

**ix)KP**: Tumbo**lo** linfanana na la mvyele**wo**

**KS**: Tumbo lako limefanana na la mzazi wako

## 4.4 Ufaafu wa Nadharia Teule

Nadharia iliyoteuliwa msingi wake ni kwamba maneno ya lugha huwa na viambishi pamoja na mizizi. Lakini hata hivyo mara nyengine hujikuta maneno yamegandana na vijipashio fulani visivyo na uamilifu wowote wa kisarufi. Inakuwa ni vinaugumu kuvichamua. Vipashio hivi ndivyo viitwavyo viangama. Kwa muktadha huu mtafiti wa kazi hii anathubutu kusema kwamba nadharia teule ni yenye kufaa kwa kiwango cha juu sana. Mawazo ya utafiti yanaonesha ya kwamba Mwanaisimu huyu alifafanua zaidi juu ya sifa za neno na kiambishi na kubainisha kuwa kuna maumbo ambayo ni tata yamechanganya sifa za maneno na viambishi na kuyaita viangama. Wakati wa uchambuzi na uchanganuzi wa vijineno hivi huwezi kubaini maana ya kisarufi ya vijineno hivyo, kinyume na vilivyo viambishi. Vipashio vilivyokozeshwa

wino katika tungo za hapo chini inaongeza mifano ya viangama vya namna na aina mbalimbali.

**Data 23**

(a) **KP**: Ndugu**zo** na kake**zo** wanpigwa

**KS**: Ndugu zako na kaka zako wamepigwa

(b) **KP**: Kanfiwa **n**dadi**ye**

**KS**: Amefiwa na dada yake

(c) **KP**: Kansema atamsumka mami**yo** kesho

**KS:** Amesema atamsuka mama yako kesho

(d) **KP**: Mjomba**wo** Kombo kazama baharini na ntumbwi**we**

**KS:** Mjomba wako Kombo kazama baharini na mtumbwi wake

(e) **KP**: Veo kanachuki na wifi**ze**

**KS**: Ve**o** ana chuki na wifi zake

(f) **KP**: Mwana**we** kagwa

**KS**: Mtoto wake ameanguka

(g) **KP**: Babi**ye** kanunua boti lya uvuvi

**KS:** Baba yake kanunua boti la uvuvi

(h) **KP:** Batuli k**a**tarudi saa**nga**?

**KS**: Batuli atarudi saa ngapi?

(i) **KP**: Kende**po** dukani kwa Mwinyi Mpeku

**KS**: Amekwenda hapo dukani kwa Mwinyi mpeku

(j) **KP:** Mgeni wetu kende**wa**?

**KS**: Mgeni wetu amekwenda wapi?

(k) **KP**: Fatuma kankoswa **m**mume**we**

**KS**; Fatma amekosewa na mume wake

(l) **KP**: Bibi**ze**, ndugu**ze** na wifi**ze** woti tawambia

**KS**: Bibi zake, ndugu zake na wifi zake wote nitawambia

(m) **KP**: Dau**lo** li**m**pwewa**vye**

**KS**: Dau lako limepwewa

(n) **KP**: Shehe kashaukata nkasi**ngwa**

**KS**: Shehe ameukata mkasi wa mtu

(o) **KP**: Hajaonja**po** zawadi za bibi**ye**

**KS**: Hajawahi kuonja zawadi za bibi yake

(p) **KP**: Mie mwanafunzi hajaniuliza**ta**

**KS:** Mimi mwanafunzi hakuniuliza hata

(q) **KP**: Kombo kankula yai**ngwa**

**KS**: Kombo amekula yai la mtu

(r) **KP**: Na**nyi** hamna**ta**

**KS**: Na nyinyi hamna hata

(s) **KP**: Kunazi**pya** zinchukuliwa

**KS**: Kunazi zote zimechukuliwa

(t) **KP**: Hwechukua**ta** mwiba sokoni

**KS**: Hukuchukua hata mwiba sokoni

(u) **KP**: Alimpiga**taa**hegutuka

**KS:** Alimpiga sana lakini hakushtuka

(v) **KP:** Mwana**o**kantoroka yupeke**ye**

**KS**: Mtoto wako ametoroka yuko peke yake

## 4.5 Baadhi ya Sentensi ambazo zinaonesha Ugumu wa Mawasiliano kwa Wageni wa Lahaja ya Kipemba

***Kipemba*: **Ndugu**zo**na kake**zo** wanpigwa

Sentensi hii haikufahamika kwa wageni wa lahaja ya kipemba , hivyo inaweza kusababisha tatizo la kimawasiliano kati yawenyeji na wageni wa lahaja hiyo.

Uangamaji uliojitokeza katika maneno *ndugu***zo** na *kake***zo**ambayo yamebeba kiangama ***zo*** ndio uliyopelekea ugumu wa kufahamika kwa sentensi hizo kwa wageni hao. Maneno haya badala yake yalikuwa yawe ndugu zako badala ya ndugu**zo** na kaka zako badala ya kake**zo**.Uangamaji wa silabi $**zo**$ umesababishwa na udondoshwaji wa mofimu //**ak**// katika maneno hayo. Hili liliendana na **nadharia***teule iliyoleta ugumu wa kiuchambuzi hivyo kupelekea ugumu wa kimawasiliano.*

*Kipemba* :Mgeni wetu kende**wa**?

Pia sentensi hii ilionekana kuwapa shida wageni wa lahaja ya Kipemba kutoka katika maeneo tofauti . Uingizwaji wa kiangama *wa* katika neno kende**wa** badala ya neno amekwenda wapi ndio uliosababisha ugumu wa kufahamika kwa sentensi hiyo.Kiangama *wa* ambacho hupatikana kwa njia ya udondoshaji wa mofimu *pi* katika neno husika na hugandamizwa katika kitenzi na hujitokeza katika hali ya kuuliza.Kiangama ***wa***hakiwezi kuchambuliwa kisarufi hivyo inaleta uumu kufahamika ninaongeza ugumu kwenye tungo na kukwamisha mawasiliano. Hali hii ina akisi moja kwa moja **nadharia** teule iliyopendekezwa.

*Kipemba*:Kunazi**pya** zinchukuliwa

Uingizwaji wa kiangama *pya* katika neno kunazi uliwatatiza wageni wengi wa lahaja ya kipemba na hivyo kupelekea kutofahamu mantiki hasa ya sentensi husika. Kiangama *pya* kimechukuwa nafasi ya neno *zote*na ndio maana neno hili likatamkwa kunazi**pya** badala ya kunazi zote.

*Kipemba* :Hajaonja**po** zawadi za bibi**ye**

Kiangama *po* katika neno hajaonja**po** badala ya neno hajawahi kuonja na kiangama *ye* katika neno bibi**ye** badala ya neno bibi yake vimewafanya wageni wa lahaja ya kipemba washindwe kupata tafsiri halisi ya sentensi hii na kuhisi kuwa Kiswahili ni kigumu hasa kipemba kwani kina misamiati ya kipekee ambayo ni tofauti na Kiswahili sanifu.

*Kipemba*: Dau**lo** li**m**pwewa**vye**

Matumizi ya kiangama *lo* katika neno daulo ,sauti //m// katika neno limpwewavye na kiangama *vye* katika neno limpwewavye yamesababisha ugumu wa kufahamika kwa sentensi hii hasa kwa wageni wa lahaja ya kipemba na badala yake maneno haya yalitakiwa kutamkika kama dau lako na sio dau**lo** , limepwewa na sio limpwewa na limepwewa badala ya limpwewavye.Hii inaonesha wazi kuwa neno dau**lo** limetokana na udondoshwaji wa mofimu *ak* na neno limpwewavye limesababishwa na udondoshwaji wa mofimu *me* na kuunganishwa kwa mofimu vye mwishoni mwa neno na kutamkika li**m**pewa**vye.**

Mfumo angami wa Kipemba huleta matatizo zaidi pale viangama vyake vinapochanganya maneno mawili na kuyafanya kuwa ni neno moja kama inavyoonekana katika baadhiya mifano  hapo juu kwa mfano:

**Data 23**

i) **KP**: Mgeni wetu kende**wa**?

**KS**: Mgeni wetu amekwenda wapi?

ii**)** **KP**: Dau**lo** limpwewa**vye**

**KS**: Dau lake limepwewa

iii) **KP**: Hajaonja**po** zawadi za bibi**ye**

**KS**: Hajawahi kuonja zawadi za bibi yake

iv) **KP**: Kunazi**pya** zinchukuliwa

**KS** : Kunazi zote zimechukuliwa

v) **KP**: Ndugu**zo** na kake**zo** wanpigwa

vi) **KP**: Ndugu**zo** na kake**zo** wanpigwa

**KS**: Ndugu zako na kaka zako wamepigwa

## 4.6 Muhtasari

Katika sura hii utafiti umefafanua mfumo angami katika lahaja ya kiswahili cha Pemba.Utafiti unaonesha kuwa mfumo angami wa Kipemba hubeba viangama mwanzoni mwa neno na mwishoni mwa neno. Hii ni kusema mfumo angami wa Kipemba unajumuisha viangama awali, na viangama tamati ambapo viangama awali vimejibainisha kuwa ni vitenzi shirikishi mbali mbali ambavyo hujitokeza katika mfumo wa silabi moja na hivyo kuangamishwa na nomino iliyopo mbele yake. na viangama tamati ni viangama vinavyofanya kazi kama ni Viwakilishi, Viunganishi, Vielezi na Vitenzi.Vilevile utafiti umefafanua kuwa kuna ugumu wa kimawasiliano kwa wageni wa lahaja ya kipemba kutokana na mfumo angami wa lahaja ya Kipemba.

# SURA YA TANO:

# MUHUTASARI WA UTAFITI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Muhutasari wa Utafiti

### 5.1.1 Muhutasari wa Kiujumla

Utafiti huu ulichunguza "***Mfumo Angami wa Kipemba na Athari zake katika Kuzuia Mawasiliano Fanisi kwa Wageni wa Lahaja hio***". Utafiti huu ulikuwa na malengo mawili ambayo niKubainisha mfumo angami wa lahaja ya kipemba na kuonesha mfumo angami jinsi unavyokwamisha mawasiliano fanisi. Utafiti huu ulifanyika kwenye wilaya ya Micheweni mkoa wa kaskazini Pemba na wilaya ya mkoani mkoa wa kusini Pemba. Kwenye wilaya ya Micheweni, shehia zilizochaguliwa ni ile ya Kwale na Kiuyu Mbuyuni. Ilhali kwenye wilaya ya mkoani shehia za Mwambe na Chokocho ziliteuliwa. Jumla ya watu themanini (80) walishiriki katika utafiti huu. Data zilikusanywa kwa kutumia mbinu za hojaji, usaili na ushuhudiaji. Data zilizopatikana zilichambuliwa kwa njia ya maelezo na majeduweli yalitumika kwa nadra sana pale yalipohitajika.

Nadharia iliyotumika katika utafiti huu niNadhara ya viangama ya Zwicky (1977) iliyofafanuliwa na Katamba na Stonham (2006). Nadharia hii itamuwezesha mtafiti kubainisha viangama katika lahaja ya Kipemba , kuainisha maneno yanayobeba viangama katika lahaja hiyo halikadhalika kuelezea jinsi viangama vinavyozuiya mawasiliano fanisi kwa wageni wa lahaja ya kipemba. Katika kubainisha maneno ambayo hubeba viangama atatutumia uchambuzi wa maneno kama ambavyo umefafanuliwana Kihore (2009) kwa sababu Katamba na Stonham wanaeleza viangama katika lugha za Ulaya.

## 5.2 Muhutasari wa Matokeo ya Utafiti

Lengo la kwanza lilionesha kwamba mfumo angami wa Kipemba unatawaliwa na vianmgama awali na viangama tamati. Viangama tamati vimejitokeza kwa wingi zaidi kuliko viangama tamati. Mfumo angami tamati wa lahaja Kipemba una aina nne kuu za viangama ambavyo ni viangama Viwakilishi, viangamaVielezi, viangama Viunganisha na Viangama Vitenzi.Viangama Viwakilishi vina maumbo ya ***ye, si,***na ***o*** maumbo ambayo ni viwakilishi nafsi ama viangama ***we, ye, ze, wo, yo***, na***zo***ni viangamaViwakilishi vimilikishi,viangama ***pya***na ***to***ni viangama Viwakilishi sifa na viangama ***nga***na ***na*** ni Viwakilishi viulizi. Kwa upande wa viangama vielezi ni ***po, mo, ko, chi***, na *wa* ambavyo ni viangama Vielezi vya pahala, viangama ***to, taa* na *je*** niviangama vya Jinsi au Namna na kiangama *nga* ni kiangama cha Idadi au Kiasi. Viangama Viunganishi vina umbo moja tu ambalo ni kiangama *ja* na viangama Vitenzi vinajumuisha maumba ya ***nda, fa,wa, ja***, na ***lya.***

## 5.3 Hitimisho

Data zimechambuliwa na kuonesha kuwa mfumo angami wa lahaja ya Kipemba upo na una viangama mbali mbali na pale unapotumika kwa wageni wa lahaja ya Kipemba husababisha muachano wa kimawasiliano. Katika uchungunguza mfumo angami wa lahaja ya Kipemba kumejitokeza aina mbili kuu za viangama, ambavyo ni viangama awali, na viangama tamati.

## 5.4 Mapendekezo

Kutokana na uchambuzi uliofanywa, utafiti huu umempa mtafiti mawazo mapana yanayomsukuma kutoa mapendekezo ambayo yatakuwa ni chachu kwa watafiti wengine wenye lengo la kufanya utafiti kuhusu viangama. Mtafiti amechambua

mfumo angami wa lahaja ya Kipemba na jinsiunavyokwamisha mawasliano kwa wageni wa lahaja hio, hivyo anaona kuwa kuna haja ya kufanywa tafiti nyingine zakuhusu mfumo angami wa lahaja hizo au kufananisha na kutofautish a baina ya mfumo angami wa lahaja ya Kipemba na mfumo angami wa lahaja nyengine.

## MAREJELEO


Anderson, S. R. (2005). *Aspects of the theories of Clicts*. New York: Oxford University Press.

Ashton, E. O. (1977). *Swahili Grammar, (Including Intonation). Singapore*: Longman Ltd

Broomfield, G. W. (1975). *Sarufi ya Kiswahili. Nairobi:* Oxford University Press.

Eastman, C. M. (1967). *An Investigation of Verbal Extention in Kenya Coastal Dialect with Special Emphasis on Ki Mvita*: Microfils Inc.

Fromkin, V. (2000). *Linguistic an Introduction to Lingustic Theory*: Blackwell Publishers Inc..

Guthric, M. (1948). *Classification of Bantu language*. London: OUP.

Guthric, M. (1967). *Comparative Bantu,an introduction to the comparative Lingustics and pre History of the Bantu language.* London: Gregg.

Hamad, K. J. (2011). "Tofauti za kiisimu baina ya Kiswahili ncha Micheweni na Kiswahili cha Wete katika kisiwa cha Pemba." Tasinifu ya Uzamili ya Kiswahili ya Chuo Kikuu Cha Tanzania.

Hinnestiusch, T. (1998).*What kind of language is Swahili?* A A P 47- 73- 95.

Ingrams, W. H. (1924). *The dialect of the Zanzibar Sultanate in bulltion of the school of oriental and Africa Studies*: London.

Katamba, F. na Stonham, J.(2006). *Mordern linguistic Morphology (2nd adition)*, Palgrave: Macmillan.

Kihore, Y. M. (2009). *Stadi za lugha ya Kiswahili sanifu*. Dar es Salaam: TUKI.

Kipacha, A. (2007). *Lahaja za Kiswahili*. Dar es Salaam: KIUTA.

Kothari, C. K. (1993). *Methodology, Methods and Techniques.* New Delh: Wiley Enstern Ltd.

Lambert, H. E. (1958). *Studies in Swahili Dialects – 11-Ki-vumba, dialect of the Southern Kenya Coast.* Kampala: East Africa Swahili Comminity. Makerere College.

Lopez, V. (2008). *Spanish Clitic Climbing. Pennisylavia*: State University haijachapishwa.

Masebo, H. (2001). *The Verb Extention in Chindali*. Dar-es-Salaam: University of Dar es Salaam haijachapishwa.

Massamba, D. P. B (1990). *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha*. Chuo Kikuu cha Dar-es- Salaam: TUKI.

Massamba, D. P.B. (2004). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha.* Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam: TUKI.

Makame M. K (2015). “Uchambauzi wa Viangama katika Kiswahili cha Mazungumzo Unguja.” Tasinifu ya Uzamili katika Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

Adi M. M (2016). “Uchambuzi wa Viangama Tamati katika lahaja ya Kitumbatu.” Tasinifu ya Uzamili katika Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

Nurse, D na Spear, T. (1985). *The Swahili reconstructing the History*. Philadelphia: Universty of Pennysylvania.

Phannuel, B. (1967). *Analysis of Tense and Aspect system in Kimachame.*University of Dar-es-Salaam (haijachapishwa).

Polome, E. C. (1967). *Swahili Language Handbook*. Centre for Applied Linguistics: Washington.

Said, D. (2011). “Viangama katika Kipemba.” Tasinifu ya Shahada ya Uzamili katika Kiswahili ya Chuo kikuu cha Dar es Salaam (haijachapishwa).

Spencer, A. (1991). *Mophological Theory an Introduction to word Structure in Generative Grammar.* London: Cambridge University Press.

Spear, T. (1999). “Early Swahili History Reconsidered Consestations and Interpretation.” Makala iliyotolewa katika semina ya Historia ya Africa SOAS. London.

Stigand, C. H. (1915). *Agrammer of Dialectical change in the Kiswahili language*. London: Cambridge University Press.

Wheeter, M. W. (1999). *Comprehensive grammer.* Routledge: London.

Whech, A. M. (1977). “On Clitics.” Indian University Linguistics Club. Bloomington.

Williman, N. (2011). *Research Methods*: *The Basic,* London and New York: Routdige Taylor and Francis Group.

# VIAMBATANISHO

## KIAMBATANISHO A

1. Badilisha sentensi zifuatazo katika lugha ya Kipemba
2. Amepita na mama yake wanakwenda mjini
3. Asha amefanana na dada yake
4. Bibi amebaki nyumbani peke yake
5. Dada zake Ali wametoroka skuli
6. Babu zake Nyona wote ni wagonjwa
7. Wamefukuzwa kazini na rafiki zake
8. Kaka yako anakwita leo
9. Babu yako Kombo amezikwa hapa Tumbatu
10. Umepita kwa mjomba wako?
11. Yule mwizi amepita wapi?
12. Hicho chakula chako nikutilie wapi?
13. Watu waliozama wamepelekwa wapi?
14. Huyo mtoto asije huko pwani
15. Amemkuta huko porini anakata kuni
16. Juma alikuwa huko Mjini
17. Babu Haji anazungumza kama mtoto mdogo
18. Ukitanda huku unaweza kupata kama kaa, dagaya na chovi
19. Ametia ndani ya ndoo
20. Amemkuta dada yake ameinama chini
21. Huyo mtoto mueke hapo chini
22. Wanafunzi wa maulidi wamekwisha kuja

23. Mgojwa wake Pandu amekwisha kufa

24. Maryam amenunua nyumba mpya jana

25. Waliporudi nyumbani wamesema nini?

26. Muheshimiwa diwani amesema sana jana

27. Mimi na yeye tumefunga swaumu

28. Arafa amezaa watoto wangapi?

29. Wanataka kwenda mjini mapema

30. Mama yake Juma hazungumzi na sisi

31. Huna mapezi na wifi yako

32. Wote wameingia garini

33. Sisi tumewatoroka askari

34. Amepigwa na mwanawe wa kumzaa

35. Mtoto huyu anafanya nini?

36. Baba zake Machano wamezaliwa kumi na mbili

37. Waliporudi nyumbani kwao wameambiwa vipi?

38. Unakwenda shamba na mke wako?

39. Mtoto amelala huko chumbani

40. Mjomba ameharisha sana jana usiku

41. Nahodha amekamata vizuri kamba ya mlingoti

42. Alipoondoka ameingia na wao gari moja

43. Nyumba hii ni nzuri sana

44. Mwalimu amevaa saa mpya

45. Paka huyu mwizi wa nani?

46. Juma amevaa nguo mpya

47. Haendi kwa ndugu zake

48. Mimi nimemuahidi mwanangu akipasi nitampa zawadi

49. Mzee aliyekuja jana amesema nini?

50. Mtoto amepigwa sana lakini hakusema

51. Zawadi hizi zimetoka kwa mkwe wako

52. Anapokuja haji na yeye

53. Mheshimiwa amesema sana mkutanoni jana

54. Baba yake mdogo ameamua nini?

55. Mtoto aliyelala amefanya nini?

56. Fatuma amekerwa na mume wake

57. Njoo nje tucheze mpira

58. Hizo embe wamechukuwa ngapi?

59. Sisi hatukujuilishwa mapema

60. Wanafanana kama wamezaliwa tumbo moja

61. Watoto hawa wamekwisha kula

62. Nyinyi muna bahati sana

63. Kuku aliyepigwa jiwe amekwisha kufa

64. Mtoto wake amepotea

65. Wageni wetu wamekwisha kuja

66. Asha amekwisha kunya

67. Ungo mkubwa umeroa

68. Amemchoma kwa ncha ya kisu

69. Mtakwenda pamoja na mimi?

70. Pesa zote zimepotea